**SERIKALI** yapokea kilio cha washusha mizigo Bandari ya Zanzibar



UKURASA 5

**MAHAKAMA** leo kutoa uamuzi anayedaiwa kujinyonga mahabusu

UKURASA 7



**WAZIRI** Mkuu aagiza TAKUKURU kuwapekua DED, Mweka Hazina utata wa malipo

UKURASA 3

SUPA JACKPOT
TZS.1,154,861,566
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Nipashe
Ijumaa Septemba 22, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581441
www.ippmedia.com
LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Simbachawene atema nyongo

**AKEMEA** mawaziri kuingia na safu zao, rushwa ya ngono kupanda vyeo, mifumo ya 'SU' kuingiliwa...
*Endelea ukurasa wa 2*

1. Harakati za kuipinga Sekretarieti ya Ajira
2. Maslahi binafsi kuhujumu TEHAMA serikalini
3. Majungu, miungu watu vimeteka kila kona
4. Ajenda ya kipekee taasisi za mishahara mikubwa



"Mbaya zaidi, unaambiwa walimpa masharti awapelekee fedha Sh. milioni tano mtoto wa kike na baadaye ikaja kutaka rushwa ya ngono..."

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene.

# Wataalamu afya washauri upendeleo bima ya watoto



UKURASA 4

UKURASA WA 11



Manispaa yabuni maboresho sokoni, huduma mahususi kwa muuzaji mwenye mtoto mgongoni

Maofisa usafirishaji hawa wapelekwe Rwanda kujifunza!

BUFE

Nipashe

Mkutano Kilimo Afrika wamuachia Dk. Samia Sh. trilioni moja za sekta

• Bashe: Kazi imeanza, miaka mitatu ijayo inaisha
• Rais aorodhesha njia zote kufanikisha matokeo

UKURASA WA 19

## CHANJO VVU KUANZA MAJARIBIO AFRIKA KUSINI

AFRIKA Kusini na Marekani zinatarajia kuanza majaribio ya chanjo mpya ya kuzuia Virusi vya Ukimwi (VVU)...

UKURASA WA 24

## GAMONDI: MUHIMU KUPATA POINTI TATU



## Wateja wa benki zilizofilisika waitwa kuchukua amana zao

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA YAIRARUA COASTAL UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Mafundi wa kampuni ya Yap Markez, wakiendelea na ujenzi wa barabara ya chini ya treni za mizigo kutoka bandarini katika eneo la Shaurimoyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Simbachawene atema nyongo

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amekemea vikali ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma, ikiwamo rushwa ya ngono.

Amebainisha kuwapo baadhi ya vigogo, wakiwamo mawaziri, wanapoteuliwa wamekuwa wakiondoa watumishi waliowakuta na kusababisha mrundikano Ofisi ya Utumishi.

Vilevile, waziri huyo ameshtukia baadhi ya taasisi na bodi kuvuruga mfumo wa ajira kwa kufanya harakati za kutaka kujitoa kwenye Sekretarieti ya Ajira, jambo ambalo alilitaja ni hujuma kwa nchi.

Waziri Simbachawene aliyasema hayo jana jijini hapa alipofungua kikao kazi cha ofisi hiyo na taasisi simamizi za maadili na mamlaka simamizi za maadili ya kitaaluma.

Alisema "Leo hii mtu akiteuliwa kuwa mkuu wa taasisi ya umma, mtu akiteuliwa kuwa waziri, kazi yake ya kwanza ili watu wamwone anafanya kazi, akifika pale ni kuanza kupangua watu. That is failure (huko ni kufeli).

"Yaani unafikaje kwenye taasisi wewe ukifika pale 'huyu simtaki, huyu simtaki'. Sasa wanajazana kwa Katibu Mkuu (Ofisi ya Utumishi) kila mtu hatakiwi na mtu mwingine, anaambiwa huyu ukifika pale majungu fitina na nini, huyu hafai, mtoe na ninyi mnasikiliza, huu ni utumishi wa umma, sio wa kwako.

"Kama ni kiongozi kweli, nenda kafanye mabadiliko kwa wale watu kwa sababu nguvu ya kiongozi ndio nguvu ya timu yake. Sasa wewe umepewa kuwa CEO (Ofisa Mtendaji Mkuu) unafika pale 'huyu simtaki, huyu simtaki'. Sasa waende wapi? Wewe wabadilishe," alisisitiza.

Waziri Simbachawene alitolea mfano kuwa alipofika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, alipewa orodha ya watu wa kuwaondoa hadi Katibu Mahsusi, lakini hakuwaondoa kwa kuwa anaamini katika kuwabadilisha.

"Tukawa tunakunywa chai pamoja ofisini kwangu, lakini pia sikutoa hata mtu. Tukafanya kazi vizuri baadaye akaletwa Kadio Katibu Mkuu tukaanza kufanya kazi vizuri, hatukuondoa mtu.

"Tumekubaliana na wenzangu pale Utumishi hawa wanaokataliwa pengine hawana pa kwenda, nyumbani kwao ni Utumishi, sisi hatuondoi mtu.

"Wakurugenzi hawa hapa, hakuna hata mmoja ameguswa, tena tumeteuliwa wote kwa pamoja. Tumewakuta tunaendelea tunawabadilisha tunakwenda.

"Hii tabia ukiteuliwa kuwa waziri au CEO wa taasisi unafika unaanza toa huyu, toa huyu, wote watoke. Hii mimi sikufundishwa hivyo niliposoma usimamizi katika rasilimali watu. Tulifundishwa unawabadilisha watu wafanye vile unavyotaka wafanye, unatoa elimu unaelezea.

"Ukiwa na wewe una majungu na wao watakuwa na majungu. Ukiwa wa haki na wao watakuwa wa haki. Sasa ukiwafukuza, watakwenda wapi? Nchi hii ni yao.

"Kwahiyo, ndugu zangu sikupanga kusema haya na pengine inaweza kuwa si sehemu sahihi niliyopaswa kusema haya, lakini nimesema ili moyo wangu upate kupona," alisema.

**KUHUJUMU MIFUMO**

Waziri Simbachawene alisema zipo baadhi ya taasisi ni kama wanagoma kuingia katika matumizi ya mifumo, wamekuwa wakisingizia mtandao upo chini.

"Wanajua watadhibitiwa, utasikia maneno makubwa ni mtandao upo chini na mahali pengine unajikuta kwenye makusanyo ya fedha kabisa watu wana fedha mikononi wanataka kulipia, utasikia 'system ipo down' (mfumo uko chini) siku ya kwanza, siku ya pili. Tunachelewesha sana maendeleo ya watu,"alionya.

Waziri huyo alisema kinachomshangaza haoni mitandao mingine kama Vodacom ikitajwa kuwa chini au kuwa na dosari za kuchelewesha malipo.

"Kuna tatizo kubwa katika matumizi ya mifumo kwenye taasisi za umma na hili si jambo zuri, lakini bado hatuchukuliani hatua kwa sababu pengine mifumo hii ina ujuzi wa wachache tu.

"Wakisema hao, wengine wote tunasalimu amri, lakini kwa uelewa wa sasa kwa mambo haya ya mifumo sidhani kwamba wakati wote wanasema ukweli, hivyo lazima tusukume hili na tuchukuliane hatua," alisema.

**UDADISI WAKE**

Waziri huyo alisema amefanya utafiti binafsi. Amegundua kuna utumishi wa umma na uongozi wa umma ambao unafanya harakati na kutafuta maslahi binafsi.

"Usawa katika maslahi ya utumishi wa umma, usawa katika hadhi, tusiposimamia hili taifa litadondoka. Lazima tuwe na mifumo wazi inayoeleza kila mtumishi kwa nafasi yake amepatikanaje na namna alivyopatikana kwa usawa na uhalisia," alisema.

**HUJUMA MFUMO AJIRA**

Waziri Simbachawene pia alisema amebaini kuna wakuu wa taasisi na bodi zinafanya harakati ya kujitoa katika Sekretarieti ya Ajira iliyoanzishwa kwa sheria, kanuni na taratibu na inafanya kazi kwa misingi ya kimataifa ili kuondoa upendeleo. "Mimi nimeapishwa nisimamie sekta ya utumishi wa umma. Si kazi yangu kujenga daraja, mimi si kilimo, mimi si (Jumaa) Awesso (Waziri wa Maji) kupeleka maji, kazi yangu kuutazama utumishi wa umma.

"Sasa kuna taasisi zinahangaika kujitoa turudi kule. Kama kuna upungufu, tuushughulikie ili ajira zetu ziwe salama. Ninahisi tunataka kufanya hujuma kwa nchi," alionya.

Waziri huyo alisema anafahamu siri ya kila mmoja kutaka kujitoa ni kwa ajili ya kwenda kutafuta apate namna ya kuajiri.

"Hivi unapata sifa gani ukiajiri wewe halafu utaajiri ndugu zako, rafiki zako? Utaajiri watu unaowataka wewe, haiwezi kuwa sawa!

"Sina hakika kama hadhara hii ni sahihi kuzungumza haya. Hivi vitu vinauma wakati mwingine ukipata mahali pa kusema unatamani upumue," alisema.

**MISHAHARA MIKUBWA**

Waziri huyo pia alisema kuna watumishi wanataka kwenda Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Benki Kuu (BoT) na Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa sababu tu kuna mshahara mkubwa.

"Wanataka kwenda BoT na huko BoT, TRA kuna upinzani wa ajabu. Hata kama unataka kumpeleka mtumishi kwa ajili ya kuongeza ufanisi, utaambiwa huko haiwezekani na imefikia sasa hata kama yupo Katibu Mkuu ambaye kazi yake ni kusimamia rasilimali watu kwa ajili ya kuleta ufanisi na utendaji bora, lakini leo akiandika barua yake iende kwenye taasisi ambayo ninyi sijui wa ununuzi sijui nani mpo, mnasema 'huyu simtaki'.

"Yupo mtumishi mmoja amefanyiwa usaili, ameshinda kwa vigezo. Akapangiwa kwenda taasisi fulani, amekwenda pale, wale maofisa utumishi wamekataa kumpokea. Wanasema wamemfanyia 'vetting' wameona hastahili kufanya pale. "Mbaya zaidi, huku unaambiwa walimpa masharti awapelekee fedha Sh. milioni tano, ni mtoto wa kike na baadaye ikaja kutaka rushwa ya ngono.

"Baadaye wakasema 'Ofisi ya Katibu Mkuu tuletewe mtu mwingine kwa sababu huyu tumemfanyia vetting'. Tunauliza huko zinakofanyika 'vetting' zinafanyika ofisi yetu, hakuna kitu cha namna hiyo," alisimulia.

Kaimu Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Xavier Daudi, alisema kuwa katika kikao hicho cha siku mbili, washiriki watajadili masuala mbalimbali na kubadilishana uzoefu kwenye utumishi wa umma ili kurudisha maadili tarajiwa ya utumishi wa umma.

## Tanzania yaainisha vivutio 6 uwekezaji

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, (Mipango na Uwekezaji), Profesa Kitila Mkumbo, ameainisha mambo sita vivutio kwa uwekezaji nchini, mojawapo ni miundombinu ya uhakika ya usafirishaji pamoja na utawala wa sheria.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa siku ya pili ya Kongamano la Tano la Kimataifa la Nishati.

Profesa Mkumbo aliwahakikishia wawekezaji na wafanyabiashara kwamba katika sekta ya nishati Tanzania ina miundombinu ya uhakika ya barabara, maji na umeme kwa ajili ya uwekezaji.

Alisema serikali inafanya jitihada kubwa ya kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ikiwamo ya usafirishaji ili wawekezaji wanapokuja wawe na uhakika wa kusafirisha bidhaa zao katika maeneo mbalimbali ya nchi na pia kusafirisha kwenda nje.

Alisema Tanzania ni nchi yenye amani na utulivu wa kisiasa, hicho ndicho kigezo namba moja kwa mwekezaji yeyote anachohitaji katika nchi husika.

Alitaja sababu nyingine kuwa ni uongozi thabiti wa Rais Samia Suluhu Hassan, anayependa uwekezaji.

Alisema Rais Samia ni kiongozi rafiki katika masuala ya uwekezaji na biashara na ndiyo maana kumekuwa na wimbi kubwa la watu wanaokuja kuwekeza nchini, hivyo ni fursa muhimu kwa kampuni au watu wanaotaka kuwekeza kwenye sekta ya nishati nchini.

Kwa mujibu wa Profesa Mkumbo, utawala wa sheria nchini ni kigezo kingine kinachowahakikishia wawekezaji usalama wa mitaji yao wanayotaka kuwekeza katika sekta ya nishati.

Alisema sheria hizo hususani za uwekezaji zimetungwa kwa kuzingatia ushauri wa wadau ikiwamo sekta binafsi na wawekezaji.

Kuhusu misingi ya kiuchumi, Profesa Mkumbo alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi chache Afrika zenye uchumi bora kwa kuwa hata ripoti ya Benki ya Dunia (WB), iliyotolewa hivi karibuni kuhusu masuala ya uchumi ilitaja Tanzania kuwa uchumi wake unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.1 katika kipindi cha mwaka 2023.

Alisema ripoti hiyo pia ilieleza uchumi wa Tanzania unatarajiwa kukua hadi kufikia asilimia sita katika kipindi kifupi kijacho.

Kwa mujibu wa WB mfumuko wa bei Tanzania utaendelea kupungua, kubakia chini ikilinganishwa na nchi nyingi jirani.

Profesa Mkumbo alisema mfumuko wa bei unakadiriwa kupungua kutoka asilimia nne mwaka huu hadi kufikia asilimia 3.9 mwaka 2025.

Pia, kijiografia Tanzania ipo kwenye eneo la kimkakati kwa kuzungukwa na nchi kadhaa ambazo ni soko muhimu, inaboresha bandari na reli.

Alisema kwa kuwa mahitaji ya umeme yanazidi kuongezeka, Tanzania inajipanga kuzalisha megawati 10,000 ifikapo mwaka 2030.

**HABARI KITAIFA**

# Waliowekeza benki zilizofilisika waitwa kuchukua fedha zao

## -Wateja FBME sasa kufidiwa fedha zao

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Bima ya Amana (DIB), imewaita wateja wote waliowahi kuwekeza kwenye benki mbalimbali zilizofilisiwa au kushindwa kujiendesha nchini waende kuchukua fedha zao.

Vilevile, imesema Tanzania imeshinda mapingamizi ya ufilisi wa benki ya FBME na mfilisi wa benki hiyo ameshateuliwa muda si mrefu matangazo yatatolewa kufidia wateja waliokuwa wakiidai benki hiyo.

Mkurugenzi wa DIB, Isaac Kihwili, alitoa taarifa hiyo jana wakati akitoa mafunzo kwa Wahariri wa vyombo vya habari, jijini Dar es Salaam kuhusu ufahamu wa kuanzishwa kwa bima hiyo ambayo ni kulinda amana za watu wanazoweka benki na kuwaongezea imani kuwa fedha zao ziko mahali salama.

Akizungumzia wateja waliowekeza amana kwenye benki zilizofilisiwa, alisema fedha zao zipo na wanatakiwa wakazichukue kwa kuwa zimekaa muda mrefu kutokana na wengine kutokuwa na uelewa wa kuzifuatilia.

"Tumejaribu kuwatafuta kwa njia mbalimbali na kupitia namba zao za simu, lakini hawapatikani, inawezekana wengine waliacha kutumia namba zao na sasa zinatumiwa na watu wengine. Wito wetu ni kuwataka waje kuchukua amana yao," alisisitiza. Alisema kwa kiwango kilichowekwa kisheria kipindi DIB ilipoanzishwa kila mteja anatakiwa kulipwa fidia ya Sh. milioni 1.5.

Hata hivyo, alisema baada ya serikali kupitia upya fidia hiyo na kuona haitoshelezi, iliamua kuongeza na kufikia kiwango cha Sh. milioni 7.5 kutokana na thamani ya fedha na uwezo wa mfuko kugharamia malipo bila shida. Kiwango hicho cha sasa hakitawahusu wateja ambao benki walizowekeza zilifilisiwa kabla ya kupitisha sheria ya kiwango kipya.

Kihwili alisema, vilevile, kuna ufilisi unaoendelea wa kukusanya mali katika benki zinazofilisiwa ili watu waweze kulipwa fedha zao.

Aliwakumbusha wateja waliokopa kwenye benki zilizofilisiwa haina maana kuwa fedha walizokopa hawatarudisha.

"Hiyo mikopo wanatakiwa wairudishe na wanatakiwa watoe ushirikiano kwa wasimamizi wa mufilisi ili ziweze kulipa fidia kwa wengine waliowekeza kwenye benki hizo," alisema.

Kuhusu ufilisi wa benki ya FMBE, alisema jumla ya madai ni Sh. bilioni 341 na wanaodai ni wateja zaidi ya 6,000. Kati ya wanaodai wapo wateja wa Tanzania na kutoka nje ya nchi.

Tanzania imeshinda pingamizi lililowekwa na Benki Kuu ya Cyprus la kuitambua DIB kama Mfilisi wa benki yote ikijumuisha makao makuu pamoja na tawi la Cyprus (Global liquidator).

Ofisa Sheria Mwandamizi wa DIB, Acley Chaula, alisema mifumo ya bima za amana ulimwenguni ilianzishwa kutokana na migogoro ya kifedha na lengo ni kuwalinda wateja wadogo wadogo wanaowekeza amana zao benki.

Alisema katika kila watu 100 wanaowekeza amana zao benki 98 wanarudishiwa amana zao zote na wateja wa bima hiyo ndio wanufaika wakubwa.

Mhasibu Mwandamizi wa DIB, Mtui Romuli, bima hiyo inafanyakazi kwa ufanisi kwa kuwa mteja anapodai amana yake iwapo benki iko kwenye ufilisi, analipwa ndani ya siku 30.

Alisema tofauti ya Bima ya Amana na bima zingine, ni kumlinda mteja na kumfanya ajiamini na kuwa na imani na sekta fedha.

# PM aagiza TAKUKURU kuwapekua DED, Mweka Hazina utata malipo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Rais Samia Suluhu Hassan akishangaa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, kushindwa kujenga jengo la mashine ya X- RAY, utata mwingine wa fedha zilizotolewa tangu mwaka 2021/22 umebainika katika Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, Kigoma.

Hali hiyo imebainika baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Zainab Mbunda, kusema fedha za miradi zipo huku Mweka Hazina wa Wilaya, Majjid Mabanga, akisema zimekwisha, kitendo ambacho kimemfanya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuagiza wachunguzwe.

Hayo yamejitokeza zikiwa ni siku nne baada ya Rais Samia katika ziara yake mkoani Mtwara kubaini halmashauri kushindwa kutenga fedha za ujenzi wa jengo hilo, hivyo kuagiza watendaji wa halmashauri na madiwani kujitathmini na kutafuta Sh. milioni 300.

Jana, Waziri Mkuu akiwa mkoani Kigoma katika wilaya ya Uvinza, alishangazwa kukuta miradi haiendi licha ya fedha kutolewa kitambo na kumwagiza Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Kigoma, Steven Mafiga, kuanza uchunguzi mara moja ili kubaini ni kwa nini miradi haiendi.

Maagizo hayo aliyatoa wakati akizungumza na watumishi na wananchi waliohudhuria uwekaji wa jiwe la msingi kwenye jengo la ghorofa moja la Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, lililoko Lugufu, mkoani Kigoma.

"Kamanda wa TAKUKURU Mkoa, kamilisha hiyo kazi kwa haraka sana. Rais wetu analeta fedha nyingi sana lakini kuna watu hawafanyi uamuzi. Mkurugenzi mtendaji na mweka hazina wakae pembeni kupisha uchunguzi wakati ukiendelea na kazi," aliagiza.

Hatua hiyo inatokana na kubaini kuwa fedha za miradi ya ujenzi wa hospitali ya wilaya, vituo vya afya vya Rukoma na Sunuka na zahanati za Mgambo na Kajeje zilizotumwa tangu mwaka 2021/2022, kudaiwa kuwapo kwenye akaunti wakati majengo husika hayajakamilika huku taarifa zinazotolewa zikisema ujenzi uko kwenye hatua ya ukamilishaji.

"Kwa nini lugha ya ukamilishaji hapa Uvinza imeshamiri? Fedha za miradi zikiletwa ziende kwenye kazi iliyokusudiwa. Sasa hapa mkurugenzi anasema fedha zipo, mweka hazina anasema zimeisha, mhandisi aliandika dokezo la kuomba vifaa, mtu wa manunuzi (ununuzi) anasema hajalipata.

"Nimewaweka pembeni kwa sababu nimeona usimamizi ni mbovu. Leo hii tukitoka Nguruka, Kamanda wa TAKUKURU ingia kazini. Angalia hizo fedha ziko kwenye akaunti zipi? Angalia kuna shilingi ngapi na zilikuwa zimepangwa kufanya shughuli gani?," alisisitiza.

Kabla ya kuweka jiwe la msingi, Waziri Mkuu alikagua hospitali ya wilaya na kubaini majengo kadhaa hayajakamilika licha ya kuwa fedha zilitolewa tangu Mei, 2021. Pia alikuta vifaa tiba vingi vikiwa kwenye chumba ambacho hakina milango wala vipoza hewa (air conditioner) huku vikiwa vimejaa vumbi.

"Ni kwa nini vifaa hivi vya kielektroniki tena vya gharama kubwa vimeachwa tu hapa, tena vinapigwa na vumbi? Hamwoni huruma kwa fedha za serikali?" alihoji. Majaliwa alisema ametembelea mikoa mbalimbali nchini na kuweka mawe ya msingi au kuzindua majengo ya wagonjwa wa dharura (EMD), lakini haelewi ni kwa nini majengo ya Uvinza hadi leo hayajakamilika. "Kibondo na Kasulu wenzenu wamekamilisha majengo yao. Iwaje hapa Uvinza bado? alihoji.

Akitoa taarifa kuhusu ujenzi wa hospitali ya wilaya, Mkuu wa Kituo kwenye hospitali hiyo, Dk. David Patrick, alisema mwaka 2019 walipokea Sh. bilioni 1.5 za ujenzi wa majengo saba, kisha wakapokea Sh. milioni 300 za njia ya watembea kwa miguu

Pia alisema Mei, 2021 walipokea Sh. milioni 500 za wodi tatu, na Machi, 2022 Sh. milioni 390 za EMD na nyumba ya watumishi na Sh. milioni 523 za vifaa tiba.

"Halmashauri ya Wilaya Uvinza ilipokea Sh. bilioni 1.5 mwaka 2019 kwa ajili ya ujenzi wa majengo saba ya awali ambayo ni jengo la mionzi, wodi ya wazazi, maabara, wagonjwa wa nje, utawala, madawa, jengo la kufulia," alisema Dk. Patrick huku akibainisha utekelezaji wa kazi hiyo ulianza Januari 10, 2019.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 115345, KIWANJA NAMBA 124, KITALU '24' KIBADA KIGAMBONI 2.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1002975 KIWANJA NA. 2483, KITALU 'A' MBEZI MANYEMA 3.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI 4. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO KINZUDI GOBA | 1.SALUM JUMA NYANDOTO 2. SALUMU JUMA NYANDOTO 3.SALUM JUMA MARWA 4.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.KIBADA- KIGAMBONI 2.MBEZI MANYEMA 3.KIGOGO KATI 4.KINZUDI GOBA | 06/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | FRANK JACKSON KASONGA | 1. NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI TMK 046855 KIBONDE MAJI " A" CHARAMBE 2.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI TMK 013567MBAGALA KIBURUGWA 3.NYUMBA YENYE HATI NA.85480,KIWANJA NA.1302 KITALU 'L' MBAGALA | FRANK JACKSON KASONGA | 1.MBAGALA CHARAMBE 2.MBAGALA KIBURUGWA 3.MBAGALA RANGI TATU | 11/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | FALLACK ADAM RUTUNGO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MADADIA ALLY SANKA | MKOLANI NYAMAGANA -MWANZA | 26/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | KOKUBELWA PAUL NGAMBEKI | KIWANJA | KOKUBELWA PAUL NGAMBEKI | MPIJI MAGOE | 28/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | SHAMSI FADHILI MASISA | NYUMBA | SAAD ADAM MDOE | KINYAMWEZI KATA YA PUGU | 06/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no**. 0715868000/ 0785242219**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

217613602



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mobhare Matinyi (katikati), akikabidhi zawadi ya nepi za kisasa kwa Rehema John aliyelazwa katika Hospitali ya rufani ya Mkoa wa Temeke, baada ya kukabidhi katoni 45 za nepi hizo kwa uongozi wa hospitali jana, kwaajili ya kusaidia wanawake waliojifungua na wanaotarajia kujifungua. Kulia ni Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Joseph Kimaro. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Wataalamu afya washauri upendeleo bima ya watoto

**Na Christina Mwakangale**

WADAU wa afya, wametoa maoni kuhusu huduma bima ya afya, hususan kifurushi cha Toto Afya Kadi, wakitaka zitengwe fedha maalumu katika bajeti ya serikali kuhudumia kundi hilo, hususan watoto kuanzia umri miaka sifuri hadi mitano.

Pia wameshauri serikali kuzingatie hilo na kulipa kipaumbele na kulindwa kisheria huku walio chini ya miaka 18 wakilindwa na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na wale walio chini ya miaka mitano wasimamiwe na Sera ya Afya ya Mwaka 2007.

Waliyasema hayo juzi usiku katika mjadala kuhusu mabadiliko ya huduma ya Toto Afya Kadi, ulioandaliwa na Mwananchi kupitia mtandao wa XSpace uliohusisha washiriki mbalimbali wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa na wananchi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Hospitali Binafsi Tanzania (APHFTA), Dk. Egina Makwabe, alisema serikali itenge fungu maalu la fedha kwa ajili ya kulihudumia kundi la la watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Dk. Makwabe ambaye pia ni daktari bingwa wa magonjwa ya mfumo wa mkojo na figo, alisema matibabu yana gaharama kubwa, hivyo kuhitaji uchangiaji na uwekezaji na Watanzania kubadili mtazamo kwa kuanza kuchangai ili kuinua kiwango cha huduma.

"Lazima kuwapo chanzo sahihi cha fedha na kuandika andiko kwa serikali itenge fedha ili kundi la watoto walio chini ya miaka mitano watibiwe kwa fungu hilo. Hili ni kundi ambalo lina magonjwa ya mara kwa mara," alisema .

Ronald Malabo, alisema watoto chini ya miaka mitano ambao bado hawajaanza shule, ndio kundi ambalo linahitaji kupewa kipaumbele, hivyo mabadiliko ya mfumo na usajili katika Toto Afya Kadi yamesababisha wengi walio katika umri huo kukosa fursa ya kujiunga.

"Mtoto wa umri sifuri hadi miaka mitano hukumsajili halafu unakwenda kumfuata mtoto huyo huyo aliyanza darasa la kwanza shuleni ajiandikishe. Mzazi hawezi kukuelewa ulipoacha kumsajili mwanawe awali uje umsajili shuleni," alisema Malabo.

Alisema serikali ianzishe mpango maalumu wa kukusanya fedha ili kuimarisha huduma ya afya nchini, hata kukata baadhi ya sehemu ya fedha za tozo.

Dk. Elisha Osati alisema akiwa mtaalamu wa afya, hukumbwa na changamoto iwapo atafika mgonjwa ambaye hana fedha ya matiababu wala bima ya afya, hivyo kuna haja ya elimu ili jamii ijue umuhimu wa kuwekeza katika afya.

"Kuwapo kampeni inayofanywa na NHIF (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya) kuhamasiha wazazi, kamati za shule, TAMISEMI (Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa) ili jamii ijiunge na bima kama ambavyo mfuko huo unatarajia kuongeza wanachama. Tunaotoa huduma ya afya tunashindwa kujua,tusimamie wapi.

"Wagonjwa wanakuja hospitalini hawana namna ya kujitibu. Wanasubiri kibali cha msamaha lakini kibali hicho hata akikipata hakiwezi kuhudumia kila kitu. Kunahitajika uamuzi wa makusudi ambao utasimamiwa na serikali. Ni lazima tuwe na uamuzi kwa sababu watu wetu wnapata taabu mno," alisema.

Naibu Msemaji wa Sekta ya Afya kutoka Chama cha ACT-Wazalendo, Ruqayya Mahmoud Nassir, alisema serikali ikae meza moja na chama hicho, ili kupata namna bora ya kutoa huduma katika sekta hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema huduma za Toto Afya Kadi hazijabadilishwa isipokuwa namna ya kufanya usajili imebadilishwa huku akisema maboresho hayo yamelenga kuongeza idadi ya wanachama.

"Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 inasema watoto ni takribani milioni 30, hivyo takribani nusu ya Watanzania ni watoto. Tulisema tuliangalie kundi hili na wamekuwa wakijiunga kwa hiari. Tulilenga kuwafikia asilimia 50 ya watoto milioni 26 idadi hii ni wakati mfuko ulipolenga kundi hilo.

"Asilimia kubwa ya hao watoto wako shuleni ndiyo maana tukabuni kifurushi kwa walioko shuleni, kwa umri wa mtoto kuanzia miaka saba na kuendelea tukiamini kwamba itawezekana. Kilichotokea kwa kiasi kikubwa wengi waliojiunga walikuwa wagonjwa. Tangu mwaka jana tulikuwa na watoto 200,000 kati ya milioni 30 ya watoto wote nchini," alisema.

Alisema mfuko huo umeendelea kutoa elimu kwa umma ingawa changamoto bado kuna familia nyingi ambazo bado hazijashawishika kujiunga kulingana na malengo ya kifurushi hicho ambacho ni maalum kwa watoto.

"Na sisi baada ya miaka mitano ya kuhudumia fao hili, tuliangalia kuna ongezeko na mwaka 2016/17 tulikuwa na watoto 24,000 lakini hadi tunasitisha walikuwa 200,000 na tukaona turudi katika msingi kwamba uwe mfumo wa kuchangiana na kupitia shule tunazo nyingi," alibainisha.

Alisema matumizi ya mfuko yamekuwa makubwa, hivyo kuna haja ya kubadili mfumo husus an katika usajili ili mapato yawe makubwa kuliko matumuzi na kwamba kwa watoto wasio na uwezo wa kuchangia upo mpango maalum kwa ajili ya kundi la watu maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

## KCMC wajivunia kuongeza mapato, kuepuka noti bandia

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuimarisha ukusanyaji wa mapato yake na kuepuka kupokea fedha bandia, Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC) iliyoko mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro, imeingia makubaliano ya kuendelea kuifanya Benki ya CRDB kuwa mtoaji wa huduma za fedha hasa ukusanyaji mapato hospitalini huko.

Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya KCMC, Prof. Gileard Masenga, amebainisha kuwa kabla hawajaanza kutumia mfumo wa benki hiyo walikuwa wanakusanya mapato kidogo na kuna nyakati walilipwa hata kwa fedha bandia.

"Kama mnavyofahamu uendeshaji wa hospitali ni wa gharama kubwa, hivyo usimamizi wa mapato ni kati ya vipaumbele muhimu vya hospitali yoyote. Ndio maana leo tupo tena hapa kuuhuisha mkataba wetu ili kuendelea kuwa na ufanisi mkubwa katika ukusanyaji wa mapato yetu," alisema Prof. Masenga jana jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi huyo alisema wahasibu walilazimika kukaa na fedha nyingi katika ofisi zao, jambo lililokuwa linawaweka kwenye hatari ya kuvamiwa, hivyo kupoteza mapato ya hospitali.

Kutokana na hali hiyo, mwaka 2014, menejimenti ya hospitali ilishawishika kuingia makubaliano na benki hiyo kutumia teknolojia ya kisasa kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato. Mfumo umeondoa makosa ya kibinadamu kwa kiasi kikubwa, hivyo kuongeza makusanyo.

Prof. Masenga pia alisema uhusiano wa Benki ya CRDB na Hospitali ya KCMC hauishii katika huduma za benki pekee, kwa kuwa wao ni miongoni mwa wanufaika wa uwekezaji unaofanywa kwa jamii na benki hiyo.

Prof. Masenga alisema benki imewajengea eneo la mapumziko kwa wagonjwa na wasaidizi wao na mara kadhaa imewasaidia vifaa tiba na kompyuta ili kuboresha utoaji huduma hospitalini.

Kutokana na makubaliana haya, sio hospitali pekee itakayonufaika na mfumo huo bali pia wale wote wanaopatiwa huduma hospitalini huko.

"Malipo sasa yatakuwa yanafanyika kutumia 'control number'. Hivyo, yeyote anayehudumiwa Hospitali ya KCMC hatahitaji kufanya malipo kwa fedha taslimu, hivyo kuweza kufanya malipo kielektroniki.

"Anayehudumiwa ataweza kulipa kwa kutumia kadi za benki ikiwamo za Visa na MasterCard, pia ataweza kutumia SimBanking, Internet banking na pia CRDB Wakala.

"Malipo haya ya kisasa yanamwezesha mfanyamalipo yeyote kulipia huduma ya kwake au ya mtu mwingine moja kwa moja hospitalini, akiwa popote alipo, ndani au nje ya nchi mradi tu awe na control number," alisema.

Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, alisema Hospitali ya KCMC ni moja ya taasisi za mwanzo kuingia ubia na benki kutumia mfumo huu wa malipo, mwaka 2014.

Ubia huo ulikwenda sambamba na uzinduzi wa kadi maalum ya malipo ya Hospitali ya KCMC iliyopewa jina 'TemboCard KCMC'.

Katika mwaka wa kwanza wa kutumika mfumo huo hospitalini huko, zaidi ya Sh. bilioni 4.1 zilikusanywa na mpaka mwaka 2022, makusanyo hayo yameongezeka mara mbili na kufika Sh. bilioni 8.7 kwa mwaka.

"Tangu tulipoingia mkataba na Hospitali ya KCMC kuanza kuutumia mfumo wetu mpaka mwaka jana, tumeiwezesha hospitali kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 52.8. Hiki ni kiasi kikubwa kukusanywa ndani ya miaka minane na makusanyo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka," alisema Raballa.

Aliongeza kuwa katika kuimarisha ushirikiano na hospitali na pia kusogeza karibu zaidi huduma kwa wateja wake, mwaka 2020 benki ilifungua tawi hospitaini huko.

Tawi hilo pia linanufaisha wafanyakazi wa hospitali, wanafunzi wanaojifunza hospitalini huko, wagonjwa, wafanyabiashra na wananchi kwa ujumla wanaoishi au kupita maeneo ya hospitalini.

000000000000000

**HABARI KITAIFA**



Mkimbiza Mwenge wa Uhuru kitaifa kutoka mkoani Manyara, Emmanuel Jackson Hondi akiukimbiza katika Mji wa Nzega, mkoani Tabora jana na kutembelea miradi mitano ya thamani ya sh. bilioni 2.5. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mtandao wa elimu waona hatari kurudi shule baada ya kujifungua

**Na Elizabeth Zaya**

MTANDAO wa Vinara wa Elimu Tanzania, umesema bado kuna hatari kwa wanafunzi waliopewa fursa ya kurejea shuleni baada ya kukatisha masomo yao kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo za ujauzito na kukatisha masomo yao.

Wadau hao wamedai kwamba licha ya serikali kuruhusu wanafunzi hao kurejea shuleni baada ya kupata ujauzito na kuweka mwongozo maalumu unaosimamia hilo, lakini bado mazingira yameonyesha kuwa huenda jitihada hiyo isiwe na mafanikio kwa kundi hilo kwa sababu vyanzo havijashughulikiwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika mkutano wao uliofanyika jana Dar es Salaam, wadau hao walisema awali miongoni mwa sababu zilizobainika wanafunzi wengi kukatisha masomo ni pamoja na ujauzito unaosababishwa na wengi wao kupata vishawishi ambavyo chanzo chake ni umasikini na kushindwa kutimiziwa mahitaji yao ya msingi.

Sababu nyingine walisema ni kutembea umbali mrefu wanapokwenda na kurudi shuleni na baadhi yao kubakwa na kupata ujauzito usiotarajiwa.

Rebecca Gyumi, ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Msichana Initiative, amesema pamoja na jitihada za serikali kurejesha wanafunzi hao shuleni baada ya kujifungua, hatari hiyo bado haijaisha kwa sababu mazingira ya awali yaliyosababisha hayajabadilika.

"Tunapongeza sana hatua na jitihada kubwa iliyofanywa na serikali katika hili la kurejesha watoto wanaopata mdondoko, na imeweka mwongozo mzuri sana unaosimamia hili, lakini mazingira ambayo yalikuwa chanzo cha shida hiyo ambayo ni kutembea umbali mrefu, umasikini na kukosa mahitaji yao ya msingi ambayo huwaingiza kwenye vishawishi vya kimapenzi na wengine kubakwa bado hayajabadilika," alisema Gyumi.

"Kwa hiyo pamoja na nia njema ya serikali kuwarejesha shuleni, bado kuna hatari ya kujikuta tunarudi kulekule, kwamba wamerejeshwa shuleni ndio kwa nia njema, lakini wakapata mdondoko mwingine kwa sababu kwa mazingira yaliyopo kuna hatari tena ya kukosa mahitaji ya msingi wakashawishika kimapenzi au kwa sababu bado wanatembea umbali mrefu wakabakwa na kupata ujauzito."

Kadhalika, alisema tatizo lingine ambalo bado linawaweka wanafunzi hao katika hatari ya kudondoka tena ni mwongozo kutokueleweka vema kwa watekelezaji namna bora ya kuwasaidia kufikia malengo yao ya kurejeshwa shuleni.

"Mfano kuna wasichana ambao baada ya kuona fursa ya kurudi shule, wao wamekuwa wakitamani kurudi kwa mfumo rasmi, lakini muongozo ambao umetoka haujafafanua kinagaubaga kwamba msichana anapochagua kwenda kwenye mfumo fulani, wale watekelezaji wanatakiwa wamsikilize kile anachokipenda," alisema Gyumi.

"Kwa hiyo unakuta kuna maeneo wasichana wanataka kurudi kwenye mfumo rasmi, lakini watekelezaji wa mwongozo ambao ni wakuu wa shule wanamwambia inabidi uende kwenye mfumo usio rasmi kwa maana ya elimu ya watu wazima. Hiyo inachangia wasichana kutokuwa kwenye mfumo ambao wao wanaupenda na wanarudi wakiwa hawajaridhika."

Pia, alisema katika utekelezaji wa mwongozo huo wa watoto kurudi shule, bado hakuna bajeti ya kutosha na ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kusaidia kutekeleza mwongozo huo.

"Sisi tumependekeza kwamba ni vema serikali itenge bajeti ya kutosha yenye mrengo wa kijinsia, kwa ajili ya kutekeleza mwongozo huu wa wasichana kurudi shule na pia ni vizuri mwongozo huo uwekwe kwenye sheria ya elimu ili iwe endelevu," alisema Gyumi.

Benedictor Mrema wa Idara ya Habari na Utetezi kutoka Shirika la HakiElimu, alisema kuna haja watekelezaji wa mwongozo huo kuufahamu vizuri ili kufanikisha utekelezaji.

"Binafsi naamini kwamba endapo kila mdau atafanya majukumu yake vizuri, huu mwongozo utawasaidia watoto hawa, na wasipouelewa vizuri tunaweza kuwa tumefanya kazi ambayo haina maana, ni wito wangu kwa serikali na wadau mbalimbali wanaohusika kila mmoja auelewe vizuri na majukumu yake na kuutekeleza," alisema Mrema.

Alitaka kuwekwa wazi takwimu za wanafunzi waliokatisha masomo na ambao tayari wamenufaika na fursa hiyo ya kurejeshwa shuleni na ufanisi wake tangu kuanzishwa utaratibu huo.

"Takwimu ziwekwe wazi kufahamu ni wanafunzi wangapi walioacha shule, kama ni wa kike ni wangapi na sababu na ni wangapi ambao wamerudi ili mwisho wa siku, serikali ijipime imerudisha wanafunzi wangapi kila mwaka, na kama kuna ambao hawajarejea ni kwa sababu gani, kama kuna kiwango kilikuwa kimewekwa na hakijafikiwa ijulikane ni kwa nini ili kuboresha," alisema Mrema.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Godliver Nkara, alisema mwaka huu wanafunzi waliorejea shuleni katika mfumo rasmi nchi nzima ni 323.

# Serikali yapokea kilio cha washusha mizigo Bandari Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Bandari Zanzibar limesema limepokea kilio cha wafanyabiashara wanaoshusha na kupakia mizigo kwa kutumia majahazi katika Bandari ya Malindi ya ongezeko la kodi baada ya kupewa mwekezaji wa Kampuni ya AGL ya Ufaransa.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Malindi, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Joseph Meza, alisema tozo zitaendelea kutumika za zamani kabla ya mwekezaji huyo hajakabidhiwa uendeshaji Septemba 18, mwaka huu.

Alisema tozo zinazolalamikiwa na wafanyabiashara hao zilipangwa kutumika toka mwaka 2018, lakini zilikuwa hazitumiki kwa ajili ya kuwapa nafuu wafanyabiashara hao.

Alisema baada ya bandari hiyo kubinafsishwa, ililazimika kukabidhi nyaraka zote za uendeshaji wa bandari, ikiwamo orodha ya bei ya utoaji na ushushaji wa mizigo.

"Tokea jana tumerejesha unafuu wa tozo na kwa sasa itatumika ile ile iliyozoeleka na wafanyabiashara na shughuli za ushushaji na upakiaji wa mizigo zimerudi kama kawaida," alisema.

Alisema serikali imezingatia hilo ili kuodoa malalamiko ya wananchi na wawekezaji hao wameshaelezwa kuwa viwango vitakavyotumika ni vilivyozoeleka na wafanyabiashara.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Nahat Muhammed, alisema kuna taratibu ambazo ziliwekwa katika kanuni za tozo za bandari toka mwaka 2018, mzigo unapoingia hupimwa uzito na hutofautiana tozo.

"Mzigo unapoingia katika bandari mara nyingi hupimwa 'volume' (ujazo) na uzito sasa kitu chochote kitakachokuwa kikubwa baina ya hayo mawili, kuna tozo fulani huingizwa huwa kama kikokotoo cha kuweza kupata jumla ya tozo ambayo mfanyabiashara anatakiwa kulipwa," alisema.

Aidha, alisema awali shughuli hizo zilikuwa zikifanyika kwa mazoea na bei zilikuwa zinatofautiana kutokana na tani za mizigo na kwamba wawekezaji hawajafanya kosa la upandishaji wa tozo isipokuwa wamefuata kanuni zilizowekwa za kibandari katika kuingiza na kutoa mizigo.

Alifafanua kuwa kasoro iliyokuwapo ni kutokaa pamoja kati ya wafanyabiashara hao na mwekezaji kuwaelekeza utaratibu wa kanuni uliopo.

Shirika la Bandari Zanzibar kwa wastani lilikuwa likipokea tani 45 za mizigo kupitia usafiri wa majahazi bandarini na hukusanya mapato wastani wa Sh. milioni 200 kwa mwezi kutokana na uingiaji na utoaji wa mizigo kupitia usafiri wa majahazi.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Idadi ndogo wanaojitokeza kupiga kura iangaliwe vyema

**MAPEMA** wiki hii, ulifanyika uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Mbarali mkoani Mbeya, uliovishirikisha vyama 12 vya siasa. Uchaguzi huo ulifanyika kutokana na kifo cha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Francis Mtega wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katika uchaguzi huo ulioshirikisha vyama 12, CCM ilitetea kiti chake na kukirejesha katika himaya yake baada ya mgombea wake, Bahati Ndingo, kuibuka na ushindi kwa kupata kura 44,334 akifuatiwa kwa mbali na Modestus Kilufi wa ACT Wazalendo aliyepata kura 10,104. Wagombea wa vyama vingine waliambulia kura chini ya 330 kila mmoja.

Vyama vingine vilivyoshiriki katika uchaguzi huo mdogo ni Alliance for Tanzania Farmers Party (AAFP), Democratic Party (DP), United Democratic Party (UDP), Chama Cha Kijamii (CCK), Tanzania Labour Party (TLP), United People's Democratic Party (UPDP), Demokrasia Makini, Union for Multi- Party Democracy (UMD), ADA- TADEA na National League for Democracy (NLD).

Pamoja na kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) yenye mamlaka ya kusimamia uchaguzi katika ngazi ya ubunge, kupitia kwa msimamizi wa mchakato huo katika jimbo la Mbarali kusema ulikuwa huru na wa haki, ACT Wazalendo kimesema kitakata rufani kwa kwenda kufungua kesi mahakamani kupinga matokeo hayo.

Hilo si jambo geni kwa sababu tangu kuwapo kwa uchaguzi unaoshirikisha vyama vingi, kupinga matokeo kwa baadhi ya vyama ni suala la kawaida na pia ni haki ya kila Mtanzania, kwa mujibu wa Katiba, kupinga katika mahakama jambo ambalo hakuridhika nalo.

Pamoja na hayo, jambo ambalo limeonekana kubwa katika uchaguzi huo na mwingine wowote uliopita, ukiwamo uchaguzi mkuu tangu mwaka 1995 ulipofanyika kwa mara ya kwanza uchaguzi ulioshirikisha vyama vingi ni kupungua kwa idadi ya wapigakura mara kwa mara. Kila uchaguzi unapofanyika, uwe mkuu au mdogo kujaza nafasi, wapigakura wanaojitokeza wanakuwa wachache tofauti na waliojiandikisha, tena kwa asilimia kubwa.

Katika uchaguzi mdogo wa Mbarali, kwa mfano, wapigakura waliojitokeza ni 56,095 kati ya 185,836 walioandikishwa katika daftari la kudumu la wapigakura ambao ni asilimia 30.4 pekee. Kupungua kwa idadi ya wapigakura katika kila uchaguzi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka hali ambayo si afya kidemokrasia.

Uchaguzi mkuu wa Rais wa mwaka 2015, mathalan, wapigakura waliokuwa wamejiandikisha walikuwa 23,161,440 lakini waliopiga kura walikuwa 15,589,639 sawa na asilimia 67.31. Kupungua kwa idadi ya watu kulionekana zaidi mwaka 2020 baada ya watu 15,091,950 sawa na asilimia 50.72 ya watu 29,754,699 kujitokeza kupiga kura. Hali hiyo inaonyesha kuwa karibu ya nusu ya watu waliojiandikisha hawakupiga kura.

Mwaka 2015 kuwapo zaidi ya asilimia 67 ya wapigakura, japo si ya kuridhisha, kulitokana na ushindani mkali uliokuwapo kati ya wagombea urais, Dk. John Magufuli wa CCM na Edward Lowassa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) aliyewakilisha Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) ulioshirikisha vyama kadhaa vya siasa. Lakini kutokana na mazingira ya kisiasa yaliyokuwapo kati ya mwaka 2015 na 2020, kulisababisha kupungua kwa wapigakura katika uchaguzi wa mwaka 2020.

Kilichoonekana Mbarali na takwimu za mwaka 2020 kitaifa, kuna kila sababu ya kurekebisha hali ili kuwezesha wapigakura wengi kujitokeza vinginevyo kuna uwezekano wa asilimia 25 ya watu kujitokeza kupiga kura. Ni vyema NEC na wadau wa masuala ya siasa wakalifanyia kazi suala hili kabla mambo hayajaharibika zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Mkutano wa Kilimo umethibitisha kwanini Mama kamteua Bashe, mkulima atajirike

Na Joseph Msindai

**CHAKULA** kina cheo kikubwa kuliko madini yote duniani hata Tanzanite na almasi haifikii umuhimu wa chakula. Kwa rais wetu, Dk. Mama Samia Suluhu Hassan ni mshindi kupendekeza kilimo namtetea kwa haya yafuatayo.

Huwezi kupika Tanzanite ili ule kama chakula, huwezi kupika almasi, iwe chakula na madini yote duniani. Utapika mahindi ukala makande, utapika mtama ule na vyakula vyote vinavyotoka ardhini (shambani) na Tanzanite, almasi vinatoka ardhini pia. Madini Tanzanite huwezi kula, 'diamond' mpaka uuze upate pesa sasa wakikosekana wanunuzi daima ni kuangukia njaa.

Hapo maana yake ni kwamba, kama hakuna hatua utaaga dunia na madini unayo mfukoni kwako na umeweka kwenye begi. Naelezea hayo, sio porojo za kudanganyana, wanasiasa, wanasheria mhudumu wao ni chakula, na binadamu wote duniani.

Hata wavivu chakula ndio uhai wa binadamu wote na wadudu wanyama kwa hiyo umuhimu ni chakula. Ubongo wangu na msaada wa Mungu ndio mawazo nilivyopewa, kwani siwezi kuringa niseme mawazo yangu mazuri.

Wasomaji watasoma kama waangalizi wa mchezo utaothaminiwa zaidi ni mpira wa miguu na kuamua kama mmeshinda au mmeshindwa watoe majawabu na ukisoma kuhusu chakula ili uwe na furaha hukosi kula kwanza asubuhi chai na mandazi au uji kama mlevi unasema nizimue ka bia.

Vinywaji hivi vimetoka shambani na 'mwenyekiti' aliyetoa jambo hili ni ardhi, wakisaidiana na jembe, mbegu na kutunza mmea usiingiliwe na manyasi na wadudu.

Ni kama wewe wazazi wa kilimo wasaidizi na wengine wengi, pia kamanda wa mbinguni mvua ni lazima bila hivyo mbegu zitakauka.

> **Utaratibu huu Mungu aliuweka na ameagiza hata asiyefanya kazi na asile chakula. Bado huruma zake tele anatuhurumia, hata kwa wavivu wanakula chakula kufanya kazi wavivu wakiwa wengi, idadi ya watu inakuwa kubwa, lakini mapato kidogo.**

Utaratibu huu Mungu aliuweka na ameagiza hata asiyefanya kazi na asile chakula. Bado huruma zake tele anatuhurumia, hata kwa wavivu wanakula chakula kufanya kazi wavivu wakiwa wengi, idadi ya watu inakuwa kubwa, lakini mapato kidogo.

Mna bahati sana kumpata mwanasiasa msema kweli, tufuate uongozi wake ili tufanikiwe. Nampongeza sana Mama Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akamteua msaidizi,Waziri wa Kilimo Hussein Bashe, ambaye uwezo wake wa siasa pande zote anastahili sifa nzuri mwenye hoja bungeni hana kelele bure, yeye ni hoja tu.

Chama chake cha Mapinduzi kimepata jembe lenye makali, sio jembe butu. Nampongeza kwa ushauri wake kwa kufuata nyayo za mkuu wake, Mama Dk. Samia, kwa uongozi na ubunifu wenye kutoa mawazo ya kusifia kilimo na kufanikisha Mkutano wa Kilimo Afrika.

Ubunifu wake umezaa matunda na sisi waandishi kujitegemea, tukakamata kalamu kuyaandika mbele ya Watanzania, ili wasome makala hii, baada ya kuiandika hivyo tunampa nguvu mbunifu Rais wetu.

Uwezo wake wa kufukiri ni mkubwa sana tunapenda watawala wengine waige mifano mingine.

**Mtunzi wa vitabu**
**+255 712 946 671**
**Dar es Salaam - Temboni**

## HABARI KITAIFA

# Kuweni tayari kwa mabadiliko - Silaa

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa amewataka watumishi wa sekta ya ardhi nchini kuwa tayari kwa mabadiliko yenye lengo la kuiboresha sekta hiyo.

Silaa alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na watumishi wa sekta ya ardhi wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ukiwa mkutano wake wa kwanza na watumishi hao tangu ateuliwe kuwa waziri.

"Tuna kazi kubwa ya kufanya mabadiliko mengi katika wizara hii ambayo yanalenga kutoa huduma kwa Mtanzania.

"Mifumo ya ICT, upimaji wetu, nchi inatakiwa kupimwa na kupangwa ili kupunguza migogoro ya ardhi," aliagiza.

Waziri Silaa aliwaambia watumishi wa sekta ya ardhi kutambua kuwa waziri aliyekuja, anafanya kazi kubwa ya kumsaidia Rais wa Tanzania katika sekta ya ardhi na lazima kufanyike mabadiliko makubwa.

Kwa mujibu wa waziri huyp, mabadiliko yanayofanyika yanalenga kutengeneza mazingira ya makazi na ardhi inayosimamiwa na wizara yake kuwa katika sura inayokwenda kumsaidia Mtanzania wa leo na miaka 50 ijayo.

Waziri Silaa aliwataka watumishi wa sekta hiyo kujitahidi katika suala la utoaji huduma bora kwa wateja hasa kauli zao wakati wa kuhudumia wateja.

"Mjitahidi majibu mnaojibu wananchi ili wawe watulivu na subira kwa kuwa inawezekana suala unalofanya liko nje ya uwezo wako, unatakiwa kumwelezea katika lugha ambayo anaweza kuelewa ili akitoka ajue, anasubiri kwa muda gani na epukeni 'njoo kesho, njoo kesho'," alionya.

Aliwahakikishia kuwa wakati wote atakuwa makini kuwalinda, lakini nao wafanye kazi ya kuwasaidia wananchi.

Silaa pia aliwataka watumishi wa sekta hiyo kuhakikisha wanapotoa huduma kwa wananchi, suala lililofika mwisho lifanyike kwa maandishi ili kuepusha matatizo.

"Jitahidi sana kuwaandikia watu jambo hili limefika hatua fulani, hiyo itatusaidia sana. Bahati mbaya sana kila mgogoro unaanza upya anapokuja kiongozi mkubwa au waziri mpya jambo linaanza upya," alihadharisha.



Mratibu wa shirika la msaada wa kisheria la Liwale Woman's Paralegal Aid Unity (LIWOPAU) mkoani Lindi, Hidaya Chikawe akitoa elimu kuhusu mambo mbalimbali ya kisheria kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Makata, mjini Liwale mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama kutoa uamuzi leo kesi anayedaiwa kujinyonga mahabusu

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kivukoni, Kinondoni, Dar es Salaam leo inatarajia kutoa uamuzi wa uchunguzi wa chanzo cha kifo cha Stella Moses anayedaiwa kujinyonga akiwa mahabusu katika Kituo cha Polisi Mburahati alikokwenda kujisalimisha.

Mahakama hiyo ilifikia hatua hiyo baada ya wajibu maombi ambao ni Mkuu wa Jeshi la Polisi na wenzake kuomba mahakama isifanye uchunguzi huo hadi pale maombi waliyoyawasilisha yatakaposikilizwa na kutolewa uamuzi. Uamuzi huo unatarajiwa kutolewa na Hakimu Mkazi, Jacqueline Rugemalila, baada ya awali kushindikana kutokana na hakimu huyo kutokuwapo mahakamani huko. Alipata dharura.

Hakimu Mkazi Janeth Kaluyenga wakati wa kuahirisha shauri hilo, alsiema hakimu anayeliendasha hakuwapo kutokana na dharura. Wakili wa waleta maombi, Peter Madeleka, alidai shauri hilo lilikuja kwa ajili ya kutolewa uamuzi na wao walikuwa tayari kuendelea.

Katika maombi ya wajibu maombi, Wakili wa Serikali Job Mrema alidai kuwa anafahamu mahakama ilitoa amri kuhusu kufanyika uchunguzi, lakini wanaomba kusikilizwa shauri jipya kwanza ndipo utekelezaji wa amri yake ufuate.

Hata hivyo, Wakili Madeleka aliomba mahakama kutupilia mbali pingamizi hilo kwa madai halina mashiko na linalenga kupotezea mahakama muda wake.

Alidai upande wa serikali haukutaja kifungu cha sheria ambacho kimekiukwa kwa kuwapo shauri hilo mahakamani.

Baada ya mahakama kusikiliza hoja za pande zote, ilikubaliana na hoja za upande wa Jamhuri na kuanza kusikiliza shauri hilo.


Stella alifariki dunia usiku wa Desemba 20, 2020, akiwa mahabusu ya Kituo cha Polisi Mburahati, alikojisalimisha baada ya kupata taarifa kuwa alikuwa anahitajika huku polisi wakidai mtuhumiwa huyo alijinyonga.

Wanafamilia hawakukubaliana na maelezo hayo. Wakaomba ufanyike uchunguzi huru kujiridhisha chanzo cha kifo hicho wakati Jeshi la Polisi likishinikiza mwili wa marehemu uzikwe.

Shauri hilo lilifunguliwa na shemeji wa marehemu, Emmanuel Kagongo, kwa niaba ya familia ya marehemu dhidi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Mburahati, Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika hati ya maombi hayo ya jinai mchanganyiko Na. 3 ya mwaka 2022, Kagongo anaomba mahakama iridhie kufanya uchunguzi huru ili kujua ukweli wa mazingira ya kifo cha ndugu yao.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Majaliwa aitaka PURA kunadi vitalu vya mafuta, gesi asilia

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameitaka Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) kuharakisha mchakato wa kunadi vitalu vya mafuta na gesi asilia nchini. Majaliwa aliagiza hayo juzi alipotembelea banda la PURA kwenye Kongamano la Nishati katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

"Hakikisheni mnaongeza kasi katika mchakato wa kunadi vitalu vyetu ili wawekezaji waje kuwekeza katika utafutaji na uzalishaji mafuta na gesi asilia nchini ili nchi inufaike," aliagiza Majaliwa.

Akitoa taarifa mbele ya Waziri Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Charles Sangweni, alisema mamlaka hiyo inaendelea na shughuli za awali za utekelezaji wa duru ya tano ya kunadi vitalu vya mafuta na gesi kwa maeneo ya nchi kavu na baharini ili kuongeza wawekezaji.

Alisema kwa sasa PURA inaendelea kuweka mipaka ya vitalu vitakavyonadiwa na kuandaa vifurushi vya data kwa kila kitalu.

Alisema mpaka sasa vitalu 26 vinafanyiwa uchambuzi kwa ajili ya kuingizwa katika mnada.

"Hadi sasa vitalu 26 vinafanyiwa uchambuzi ili kupendekezwa kwa ajili ya kuingizwa katika mnada na kati ya hivyo, vitalu 15 vipo nchi kavu na 11 baharini," alisema Sangweni.

Sangweni alisema serikali inatarajia kuzindua rasmi kazi ya kunadi vitalu hivyo kati ya Desemba mwaka huu na Machi mwakani baada ya kukamilika shughuli za maandalizi zinazoendelea.

"Kazi hiyo ya kunadi vitalu inakadiriwa kugharimu jumla ya Sh. bilioni 3.5 na kwa mwaka 2023/24 serikali kupitia PURA imetenga Sh. milioni 500 kwa ajili ya kazi za awali za maandalizi ya kazi hiyo," alifafanua Sangweni.



Mkurugenzi wa Masoko na Ubunifu wa Serengeti Breweries Ltd, Anitha Msangi Rwehumbiza, akifafanua jambo katika uzinduzi wa tamasha la utamaduni wa Kitanzania la Oktobafest 2023 kwa vyombo vya habari, jijini Dar es Salaam juzi, linalotarajiwa kufanyika Oktoba 21 mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu 12 wa VETA kupewa ufadhili mafunzo nje ya nchi

**Na Joseph Mwendapole**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetia saini mkataba na taasisi ya kimataifa ya GFP utakaowezesha walimu 12 wa vyuo vya ufundi stadi nchini kwenda nje ya nchi kupata elimu ya juu ya uungaji vyuma ili wapate vyeti vinavyotambuliwa kimataifa.

Mkataba huo ulitia saini juzi katika ofisi za Makao Makuu ya VETA Dar es Salaam baina ya Mwanzilishi wa GFP, Michael Vallez na Mkurugenzi wa Elimu ya Ufundi wa Wizara ya Elimu, Dk. Noel Mbonde.

Baada ya kutia saini makubaliano hayo, Dk. Mbonde alisema asasi hiyo ya Marekani ambayo inatoa misaada katika sekta ya elimu, itatoa elimu kwa wakufunzi wa VETA kuhusu uchomeleaji vyuma ili wapate vyeti vitakavyokubalika kimataifa.

Alisema Tanzania ina miradi mingi ya ujenzi kama Bwawa la Uzalishaji Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), reli ya kisasa na bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi mkoani Tanga. Yote inahitaji wataalamu.

Alisema kuwa katika miradi hiyo mikubwa, idadi kubwa ya wanaofanya kazi ni wataalamu wa kigeni na Watanzania ni wachache kwa kuwa wengi wao wana vyeti ambavyo havitambuliki kimataifa.

"Wenzetu wanapokuja kujenga miradi mikubwa, wanataka wataalamu wenye vyeti vinavyotambulika duniani.

"Sasa ili kuondoa hilo ombwe, hawa GFP wameamua kufundisha vijana wetu wa VETA nje ya nchi, wengine Afrika kusini, wengine Marekani kusomea uungaji vyuma," alisema

Alifafanua kuwa baadhi ya walimu watakaa katika nchi hizo kwa miezi tisa na wengine mwaka mzima na watakaporejea watakuwa na ujuzi wa hali ya juu wa uunganishaji vyuma na watapatiwa vyeti vinavyotambulika kimataifa na wataajiriwa kwa urahisi kokote duniani.

"Wakirudi watawafundisha vijana wanaosomea fani hiyo nchini ili nao wapate ujuzi kama huo na kutambuliwa kimataifa. Awamu ya kwanza watakwenda wanne, wakirudi watakwenda wengine wanne mpaka wafikie 12," alifafanua.

Alisema wakati hayo yakifanyika, serikali nayo itakuwa inaandaa karakana za ufundi za Tanzania ili zifikie viwango vya kimataifa. "Kusomesha watu wengi nje ya nchi ni gharama kubwa sana, lakini kupitia walimu hawa na karakana ambazo zinatambuliwa kimataifa, vijana wetu watasomea nchini," alisema.

Dk. Mbonde alisema serikali kwa sasa inazingatia zaidi mafunzo ya ujuzi na ndiyo sababu imefanya mabadiliko ya mitaala kuanzia elimu ya awali mpaka kidato cha sita, itakuwa ikizingatia zaidi elimu ya ujuzi.

Alisema lengo la serikali ni kuwawezesha wanafunzi katika kila hatua watakayopitia wawe na ujuzi utakaowawezesha kujiajiri wenyewe badala ya kuhangaikia ajira.

Mnufaika wa mafunzo hayo kutoka VETA Mbeya, Patrick Ngailo, alisema kupitia mradi huo, taifa litapata wataalamu wengi na kuzalisha wachomeleaji vyuma wasiopungua 5,000.

Alisema watakapomaliza mafunzo watatawanywa maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi na wanatarajia kunufaika kwa kupata kazi kwenye miradi mikubwa ya serikali kama JNHPP na reli ya kisasa.

# RC Shigela apongeza udhamini maonesho madini, 400 kushiriki

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martin Shigela ameipongeza Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kuendelea kuwa mdhamini mkuu wa Maonesho ya Sita ya Teknolojia ya Madini Geita ambayo mwaka huu yanashirikisha zaidi ya washiriki 400.

Ametoa pongezi hiyo baada ya maonesho hayo kuzidi kuwa na mvuto na kushirikisha washiriki kutoka nje ya nchi ikiwamo Burundi, China, India na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Shigela alitoa pongezi hizo alipozungumza na waambia waandishi wa habari jana mjini hapa kuhusu maonesho hayo yanayofanyika katika Viwanja vya Bombambili mjini Geita, yamekamilika. Mwaka jana washiriki walikuwa zaidi ya 250.

Alisema Mkoa wa Geita umeweka mazingira mazuri kwa kampuni zinazojihusisha na utafiti wa madini, uchimbaji unaotumia teknoljia rahisi, uchenjua na uongezaji thamani ili kuwasaidia wachimbaji wadogo kukua kibiashara.

"Niwakaribishe wawekezaji kuwekeza viwanda vya uchenjuaji na uongezaji thamani ili kuwaelimisha wananchi na wachimba wetu kuondokana na matumizi ya kemikali hatari kama vile zebaki.

"Pia niwakaribishe wananchi wote hasa wanaojihusisha na uongezaji thamani. Niwaombe waje kwa wingi kwa sababu maonesho yalianza jana (juzi) tarehe 20 Septemba 2023," alisema.

Mkuu wa Mkoa alisema maonesho hayo yatafunguliwa rasmi kesho na Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko ambaye pia ni Waziri wa Nishati. Maonesho hayo yatafungwa na Rais Samia Suluhu Hassan tarehe 30 Septemba 2023.

Akizungumzia ushiriki wa GGML katika maonesho hayo mjini Geita jana, Meneja Mwandamizi wa kampuni hiyo anayesimamia uhusiano wa jamii, Gilbert Mworia, alisema maonesho hayo yamekuwa na mvuto wa kipekee tangu yalipoasisiwa kutokana na ufadhili wa GGML kupitia mfuko wa uwajibikaji kwa jamii (CSR) ambao uliwezesha ujenzi wa eneo hilo la EPZA pamoja na eneo la uwanja huo wa maonesho.

Amesema GGML imekuwa kinara wa kuboresha maonesho hayo kwa kuwekeza Sh. milioni 800 katika ujenzi wa jengo la utawala la EPZA.

"Msaada wetu unavuka usaidizi wa kifedha ambao tumeendelea kuutoa kila mwaka, kwa sababu tulitoa msaada wa maandalizi ya maonesho hayo kama vile mahema, jenereta la dharura na mafuta yanakayotumika kwa wakati wote wa maonesho," alisema Mworia.

Alibainisha kuwa ili kutimiza malengo ya muda mrefu ya ukuaji wa uchumi endelevu, GGML inaunga mkono Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Wanalenga kuiwezesha sekta ya uchimbaji madini kukua na kufikia kiwango cha asilimia 10 katika Pato la Taifa.




Kaimu Mkurugenzi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mbaruku Magawa (kushoto), akikabidhi zawadi ya mti kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela ikiwa ni moja ya kampeni za mfuko huo, wakati wa ufunguzi wa semina ya maandalizi ya kustaafu kwa wastaafu watarajiwa wa mfuko huo, jijini Arusha jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Madereva wenye makosa 20,000 ya barabarani washughulikiwa

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

KATI ya Januari hadi Julai mwaka huu, Jeshi la Polisi mkoani Manyara limeyafanyia kazi makosa ya usalama barabarani 20,905, huku kesi 47 zikifikishwa mahakamani.

Katika makosa hayo, madereva wawili wa mabasi makubwa ya abiria yaendayo mikoani, wametiwa hatiani mahakamani na kufungiwa leseni kwa kosa la uendeshaji wa hatari.

Hayo yamo katika taarifa ya utendaji wa jeshi hilo iliyotolewa na Kamanda wa Polisi mkoani Manyara, Kamishna Msaidizi George Katabazi.

Alisema katika operesheni zao, wamekamata pikipiki 73 zilizokuwa zimefungwa taa zenye mwanga mkali, ambao ni hatarishi kwa watumiaji wengine wa barabara, hasa nyakati za usiku na ni kinyume cha Sheria ya Usalama Barabarani.

Kamanda Katabazi alisema taa hizo zimesababisha ajali nyakati za usiku na alidai walikamata pikipiki tatu zilizokuwa na mabomba ya kutolea moshi inayotoa milipuko ambayo husababisha taharuki na hofu kubwa kwa wananchi na watumiaji wengine wa barabara.

Vilevile, alisema hatua kali za kisheria zimechukuliwa dhidi yao ili kudhibiti vitendo viovu.

Kutokana kamatakamata hiyo, baadhi ya wakazi wa Babati, waliozungumza na Nipashe, akiwamo Asha Iddy. walisema polisi wamefanya vizuri kwa kuwa pikipiki hizo zilikuwa kero kubwa mjini na zimesababisha watu wengine kuugua shindikizo la damu.

Mkazi wa Mtaa wa Majengo Mapya, Simon Joseph, alisema polisi wamefanya jambo zuri. Linapaswa kuwa endelevu ili tabia hiyo ikomeshwe.

Mkazi wa Maisaka A, Amina Ibrahim, alisema kukamatwa kwa pikipiki hizo ni halali kwa kuwa zinaondoa usikivu kwa watu na kuathiri afya.

# RC ampa siku 11 DED kutengeneza mtambo ulioegeshwa mwaka mzima

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella amempa siku 11 Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Seleman Msumi kutengeneza mtambo wa kuweka vizuri barabara.

Mtambo huo umeegeshwa katika ofisi za halmashauri hiyo kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa.

Mongella alitoa maagizo hayo juzi alipozuru wilayani humo kutokana na miundombinu ya halmashauri hiyo kuwa na hali mbaya, ikiwa ni pamoja na barabara zinazokwenda kwenye taasisi za serikali kutopitika.

"Haiwezekani Mkurugenzi wa Halmashauri hii mna mitambo yote ya kutengeneza barabara hadi malori, halafu barabara zote za halmashauri yako za ovyo, zimeoza hazipitiki.

Ninakuagiza Oktoba Mosi mwaka huu mitambo hii iwe imetengemaa na ianze kufanya kazi ya kutengeneza barabara.

"Ninasema hivi kwa sababu hamtendi haki kwa wananchi. Haiwezekani wananchi wanapita barabarani wanaona mitambo imeegeshwa hapa haifanyi kazi ilhali wanakabiliwa na adha kubwa kutokana na miundombinu mibovu ya barabara. Picha ya serikali kwa wananchi inakuwaje?" Mongella alihoji.

Kwa mujibu wa Mongella, halmashauri hiyo ilinunua mitambo hiyo kwa ajili ya kutengeneza barabara huku wakijua kuwa itahitaji matengenezo, lakini hawatengenezi fedha kwa ajili ya kutengeneza mitambo hiyo.

"Kwenye miti hakuna wajenzi. Hii siyo halmashauri ya kwanza nchini kuwa na mitambo. Halmashauri nyingine zina mitambo na inafanya kazi muda wote.

"Mimi sikuelewi mkurugenzi, haiwezekani ukae mwaka mzima bila kutenga bajeti ya kutengeneza mitambo. Mitambo ni mashine zinazohitaji kutengenezwa kila siku kutokana na tija yake, siyo ya kusubiri bajeti," alionya.

Vilevile Mkuu wa Mkoa alisema kuna mchezo mchafu unachezwa ili zabuni za kutengeneza barabara zipewe makandarasi kwa maslahi ya watu ambao wameshajitengenezea njia ya kupata fedha.

"Hapa tatizo kubwa mimi ninalijua, watu wanataka zabuni wapewe makandarasi kutengeza barabara.

Unaweza kukuta ni mtandao mrefu wa kuhakikisha kwamba halmashauri haitengenezi barabara wala Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kutokana na 'chain' (mnyonyoro) waliyojitengezea kutiptia kampuni zao ili wapate fedha," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wa Kata ya Oldonyosambu, Jackson Lengojio, alisema wanakabiliwa na changamoto kubwa ya barabara ambapo wanawake wengi wanajifungulia nyumbani na wakati mwingine kupoteza maisha kutokana na ubovu wa barabara.

"Sisi wananchi tunamwomba Rais Samia Suluhu Hassan atusaidie tupate barabara. Hali ni mbaya, tunakodisha magari kwa ajili ya kuwapeleka wake zetu kujifungua, yanakwama wanajifungulia njiani na wengine wanapoteza maisha.

"Inasikitisha mno barabara zetu hazipitiki halafu tukienda ofisi za halmashauri, tunakuta mitambo imeegeshwa haifanyi kazi. Hii si sawa, wananchi wa vijijini tunateseka barabara zimejaa makorongo na vumbi linalotuletea maradhi," alisema.

Paulo Mebooki, mkazi wa Kijiji cha Osinoni Juu, alisema wanakabiliwa na adha ya barabara. Inachangia kukwamisha miradi ya maendeleo kwa kushindwa kupeleka vifaa vya ujenzi.

"Wananchi tunateseka wakati mwingine tunalazimika kubeba kwa vichwa vifaa vya ujenzi wa nyumba zetu na za kutekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo yetu," alilalama.

Mkurugenzi Mtrendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Msumi, aliahidi kutenga fedha kwa ajili ya kutengeneza mitambo hiyo na Oktoba Mosi mwaka huu itakamilika.

# Viongozi wa CCM wapewa angalizo miradi chini ya kiwango

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) , Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, amewataka viongozi wa chama hicho kuanzia ngazi ya chini, kusimamia kwa karibu miradi inayotekelezwa na serikali katika maeneo yao ili iwanufaishe wananchi.

Noel Severe aliagiza hayo juzi alipofanya ziara ya kamati ya siasa ya chama hicho kukagua miradi ndani ya Kata ya Sokon 11.

Alisema serikali imekuwa ikitoa mamilioni ya shilingi kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali, lakini changamoto iliyopo ni baadhi ya viongozi kutosimamia kikamilifu miradi hiyo, ili kutekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa.

"Tumetembelea miradi mbalimbali katika kata hii, ikiwamo ujenzi wa bweni la Shule ya Sekondari Oldadai, Kituo cha Afya Ng'iresi na jengo la utawala la shule hii.

"Tumebaini upungufu mwingi, ikiwamo kusuasua miradi hii kwa sababu ya kutotumia fedha za serikali ipasavyo na baadhi ya miradi kutekelezwa chini ya viwango. Ni jambo ambalo halikubaliki," alionya.

Alipongeza kukamilika mradi wa daraja na barabara ya Kiutu na Sokoni II ambayo awali ilikuwa ni changamoto kubwa baada ya kusombwa na mafuriko na kusababisha kukosa mawasiliano baina ya kata hizo.

Aliwataka viongozi hao kuwa na huruma na fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi na kuwa mstari wa mbele kukemea pale wanapobaini miradi kutekelezwa chini ya kiwango.

Diwani wa Sokon 11 wilayani Arumeru, Obedi Melami, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya kutatua kero mbalimbali za wananchi, ikiwamo katika kata hiyo ambayo imepewa Sh. milioni 438 kwa ajili ya ujenzi wa daraja linalounganisha kata ya Kiutu na Sokon 11 baada ya daraja lililokuwako kuzolewa na mafuriko.

Melami alisema ujenzi wa daraja hilo ulianza Juni 6 mwaka huu na kukamilika kwa daraja hilo kutaleta mafanikio makubwa kwa wananchi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Baadhi ya wananchi walipongeza serikali kwa kuwasaidia ujenzi wa daraja hilo na miradi mingine mingi, wakitaka iendelee kutenga fedha zaidi kwa ajili ya miradi ya kata hiyo.





# RPC Mutafungwa ateta na wananchi

**Na Elizabeth Seleman,**
SENGEREMA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Willbroad Mutafungwa, ameendelea na ziara yake ya kukutana na wananchi wanaoishi katika maeneo ya pembezoni mwa mkoa huo, lengo likiwa ni kubaini kero zao za kiusalama na kuzitafutia ufumbuzi.

Katika ziara yake hiyo, Kamanda Mutafungwa aliwaomba wananchi kuongeza nguvu katika ulinzi shirikishi huku akiwataka askari wenzake kutilia mkazo ushirikishwaji wa wananchi.

Akiwa katika Halmashauri ya Buchosa wilayani Sengerema juzi, Kamanda Mutafungwa alitoa mbinu za kukabiliana na uhalifu kupitia ulinzi shirikishi huku akikemea vitendo vya wananchi kujichukulia sheria mkononi na kuhakikisha taarifa zote za uhalifu zinafikishwa katika vyombo vya sheria.

Kamanda Mutafungwa aliwataka Polisi Kata kuanzisha vikundi shirikishi vitakavyosaidia kudhibiti uhalifu, pia wananchi wanatoa taarifa za wahalifu wanapowakamata.

"Jeshi letu halitavumilia kuona vitendo vya uhalifu vikiendelea kutokea katika jamii. Lazima sheria ichukue mkondo wake maana wilaya hii imeonekana kuongoza kwa kuwa na matukio kila uchao, niwaombe achene mara moja,"alionya.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Mwanza, Mkaguzi wa Polisi Faraja Mkinga, alitaka wananchi kuacha kumalizana wao kwa wao kufuatia matukio ya ukatili ambayo ni pamoja na ukatili wa watoto, ubakaji na ulawiti kwa kuwa kufanya hivyo kunamnyima haki za msingi yule aliyefanyiwa kitendo husika.

Pia aliwakumbusha wazazi kushiriki kikamilifu katika malezi bora kwa watoto ili kuwalinda na kuwaelimisha kuhusu mazingira hatarishi na vitendo vya ukatili wanavyoweza kufanyiwa nyumbani au shuleni.

Akitoa taarifa ya matukio wilayani mwake, Mkuu wa Polisi Wilaya ya Sengerema, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi Mohamed Haji, alisema katika kipindi cha Januari mpaka Septemba 2022, walirekodi makosa 245 huku Januari hadi Septemba mwaka huu kukiwa na jumla ya makosa 169.

Alisema kuwa kati ya makosa hayo, yamo ya ubakaji, lugha za matusi, kutelekeza watoto, kutupa watoto, shambulio la aibu, kufanya mapenzi na kuwapa mimba mwanafunzi, ulawiti, kutekeleza familia na ukeketaji.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Bukokwa walilishukuru jeshi hilo kwa kuendelea kuimarisha ulinzi kuanzia gazi ya kata kwa kuwa awali vitendo vya kihalifu vilikuwa vimezidi kulinganisha na sasa. Ulinzi uendelee kuimarishwa ili kutokomeza kabisa vitendo hivyo.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, ACP Janeth Magomi akionyesha kwa waandishi wa habari mkoani humo jana, silaha aina ya shortgun yenye namba za usajili TZ CAR 69657A, iliyokuwa ikitumika katika matukio ya uhalifu, iliyotelekezwa na wahalifu baada ya kugundua kuwa wanafuatiliwa na polisi, wakati wa msako maalum uliofanyika hivi karibuni ambapo watuhumiwa 12 walikamatwa. **PICHA: MARCO MADUHU**

## RC anyoshea kidole SUMA JKT kuchelewesha mradi

**Na Marco Maduhu,**
KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme amekerwa na ucheleweshwaji mradi wa ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama.

Ni mradi unaotekelezwa na mkandarasi SUMA JKT, Mkuu wa Mkoa akiagiza mkandarasi aongeza kasi ili huduma zitolewe katika jengo hilo.

Jengo hilo kwa sasa ujenzi wake umefikia asilimia 30, nyuma ya matarajio – ulipaswa kuwa umefika asilimia 35. Unatakiwa kukamilika na kukabidhiwa mwanzoni mwa mwaka 2025.

Mkuu wa Mkoa baada ya kukagua mradi huo juzi, aliagiza kasi iongezwe ili kuendana na matarajio ya ujenzi wake.

"Fedha za ujenzi wa jengo hili siyo tatizo, serikali imetoa fedha, hivyo hakuna sababu ya mradi huu kuendelea kuchelewesha kukamilika.

"Niwaagize sasa SUMA JKT, ongezeni kasi, mwongeze wafanyakazi na mfanye kazi usiku na mchana," aliagiza.

Mndeme alisema serikali inataka kinamama wajisikie raha wanapokuwa wanajifungua na kujifungua salama, Ndio ya sababu ya kuendelea kuboresha huduma za afya.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kahama, Thomas Muyonga, alisema jengo hilo ni muhimu katika kuhakikisha kinamama wanajifungua salama. Mradi ukamilishwe ndani ya muda.

Msimamizi wa mradi wa ujenzi huo kutoka SUMA JKT, James Saimon, alimwahidi Mkuu wa Mkoa watajenga usiku na mchana. Watakamilisha mradi ndani ya muda.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Dk. Shani Mudamu, akisoma taarifa ya ujenzi huo, alisema unatarajiwa kukamilika mwaka 2025, ukigharimu Sh. bilioni 6.7 chini ya mkandarasi SUMA JKT.

Baadhi ya kinamama wa Kahama wameipongeza serikali kwa kuendelea kuboresha huduma za afya na kuwasogezea huduma hizo karibu na makazi yao, hivyo kuwa na uhakika wa usalama wa afya zao, hasa kujifungua salama.

# Watumishi kizimbani kwa mashtaka ubadhirifu Mil 409/-

**Na Jenesta Jasson,** BUKOBA

WATUMISHI watatu wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, mkoani Kagera, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kagera wakikabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi na ubadhilifu wa fedha za umma Sh. milioni 409.

Watumishi hao wanadaiwa kutoa leseni bandia kwa wafanyabiashara na kuisababishia hasara serikali.

Katika kesi hiyo, washtakiwa ni aliyekuwa Ofisa Biashara wa Manispaa hiyo, Richard Kubona, Adelina Kasigwa na Mussa Kalumba. Watuhumiwa hao walipandishwa kizimbani juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Janeth Masesa na kusomewa mashtaka yanayowakabili na mawakili wa upande wa Jamhuri; Kelvin Murusuri na Jacob Daudi.

Akisoma hati ya mashtaka hayo, Wakili wa Jamhuri Kelvin Murusuri alidai watuhumiwa hao wanakabiliwa na makosa mbalimbali ya uhujumu uchumi, ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka.

Alidai watumishi hao walishiriki katika ubadhirifu, ufujaji na matumizi ya nyaraka feki kumdanganya mwajiri kinyume cha vifungu vya sheria namba 22, 23 na 31 vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Wakili huyo alidai watuhumiwa wa hao wanakabiliwa na shtaka lingine la kughushi nyaraka za serikali kinyume cha sheria.

Hata hivyo, washtakiwa hao hawakurusiwa kujibu chochote dhidi ya mashtaka hayo kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka kisheria kusikiliza kesi hiyo, vinginevyo ipewe rukhsa na Mahakama Kuu.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Oktoba 4 mwaka huu itakapotajwa tena. Washtakiwa walipelekwa rumande.




Ukurasa 13

Maofisa usafirishaji hawa wapelekwe Rwanda kujifunza!



## Manispaa yabuni maboresho sokoni, huduma mahsusi kwa muuzaji mwenye mtoto mgongoni

Ukurasa 14


BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 22, 2023

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe


# Mkutano Kilimo Afrika wamuachia Dk. Samia Sh. trilioni moja za sekta

- Bashe: Kazi imeanza, miaka mitatu ijayo inaisha
- Rais aorodhesha njia zote kufanikisha matokeo

**Na Renatha Msungu**

BADO Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, yuko katika ngazi ya kung'ara kwenye sekta ya kilimo kimataifa, pale anapoonyesha mageuzi makubwa, hata kukubalika kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mifumo ya Chakula Barani Afrika, mwaka huu.

Ni juzi tu ndani ya falsafa hiyo kuenda na kilimo cha kisasa kujitosheleza kimahitaji na kibiashara, Rais akaonyesha hoja kwa vitendo, pale alipokuwa anamaliza ziara yake kutoka mikoa ya Kusini, akiwa Ikwiriri Rufiji, akaja na mkakati unaoendelea wa serikali kulitumia bonde la Rufiji, kuwekeza skimu ya kuzalisha hekta 3,000 za mpunga.

Hapo akafafanua kwamba, zao hilo kama zilivyo mbaazi na ufuta, zina soko kubwa kimataifa, hoja ambayo kimsingi inaendeleza simulizi ya yatokanayo katika mfululizo wa yaliyojiri mkutano huo wa kilimo Afrika, jijini Dar es Salaam, mwezi huu.

Serikali pia ikalenga kutumia mkutano huo, kupata fedha kutoka kwa wadau mbalimbali, ili kuendeleza maeneo mbalimbali ya sekta kilimo nchini.

Moja ya maeneo inayolenga, inajumuisha Programu ya Vijana ya Jenga Kesho Kilimo iliyo Bora (BBT), kilimo cha umwagiliaji, uboreshaji miundombinu, pamoja na kilimo cha matunda na mboga, ikiwamo miradi ya Legas, ambavyo vyote vilikuwa ajenda iliyopitishwa na Bunge katika Bajeti ya Sekta Kilimo kwa mwaka wa fedha uliopo.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akikata utepe moja ya nakala zinazoonyesha fedha ambazo wametia saini kwa ajili ya mkopo uliotolewa na Benki ya Dunia, Tanzania ikinufaika na Mkutano wa Kilimo wa Afrika, uliofanyika Dar es Salaam, mwezi huu. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

Katika mkutano wa mwaka huu uliomalizika, ulipata mahudhurio ya watu 5,000 katika ukumbi Julius Nyerere (JNICC), badala ya 3,000 iliyotarajiwa awali, ikiwa ni wastani wa asilimia 166.6 ya matarajio hayo.

Taarifa za mkutanoni zinaainisha kwamba, kati yao wamo wakulima wadogo na wafanyabiashara wa nchini, pia watu 2,000 kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika wameshiriki.

Uwapo wa wageni unatajwa kuwa nao ni sehemu ya 'Utalii Mkutano', watu wanakusanyika nchini kuzuru mahali hapo.

Pia, taarifa zinaonyesha kwamba,katika hilo, taarifa za majumuisho taifa limefanikiwa kutokana na kupata fedha za mikopo ya muda mrefu, zaidi ya shilingi trilioni moja, kutoka kwa wadau mbalimbali.

Ni fedha zinazoelekezwa kuboresha sekta ya kilimo, ili wakulima wafanye kwa tija, kwa matarajio itawainua kiuchumi, pia zao lake linachangia pato la taifa kiuchumi.

Hapo nako, taarifa ya yatokanayo na mkutano huo unaopaisha wasifu wa Rais Dk. Samia, uchumi wa nchi unatajwa kusonga kuelekea kilimo biashara, hali kadhalika kushawishi vijana na wanawake kujiunga na sekta hiyo.

Wadau waliotoa mikopo, wanajumuishwa ni Benki ya Duniani (WB), Benki ya Maendeleo Afrika (ADB), benki ya nchini CRDB, AGRA, Agricom na wadau wengine wametia saini mkataba wa kutoa vifaa vya kisasa kwa sekta kilimo, kama vile trektra.

Ni mkutano uliohudhuriwa na marais zaidi ya watano kutoka Afrika, viongozi wastaafu, mawaziri na wawakilishi kutoka mataifa 70 barani Afrika, umezidi kuitangaza Tanzania katika ramani ya dunia, mahsusi kwenye sekta kilimo.

Waandaaji wa mkutano, Shirika la Kimataifa la Mifumo ya Chakula (AGRA), kwa kushirikiana na serikali, wanataja mafanikio makubwa yameletwa nchini.

Rais wa Shirika la Kimataifa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRA), Dk Agnes Kalibata, anatamka kufurahishwa na ushirikiano waliopata baina yao na serikali chini ya Rais Dk. Samia, akitaja ni ishara serikali imedhamiria kuzidi kukiinua kilimo.

Pia, analitaja ni jambo ambalo wao AGRA wanaliridhia na wataendelea kutoa ushirikiano kwa serikali nchini, akiwahakikishia wakulima kuendesha kilimo chenye manufaa kwa taifa, ikiwamo kuchangia pato la taifa.

**WAZIRI BASHE**

Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo, anakumbusha maudhui ya mkutano, ikiwamo hoja ya Rais Dk. Samia, kwamba wakulima wa Afrika hawahitaji kusaidiwa, isipokuwa wanahitaji haki ya keki ya dunia, ili waweze kujitegemea kuinua kilimo chao.

Anawatafsiri wakulima kwamba ni wafanyabiashara na si watu wa kusaidiwa, hivyo moja ya mikakati wamejiwekea ni kuhakikisha wanaenda kuimarisha suala sekta katika sura pana, ikiwamo mifumo ya chakula, ili Tanzania iwe kinara katika uzalishaji chakula Afrika, ikiwezekana pia katika baadhi ya maeneo duniani.

"Kwenye hili kiukweli tumeweka mikakati, mimi na mawaziri wa kilimo wa nchi nyingine, kuhakikisha tunaimarisha sekta ya kilimo. Ndio maana unaona tumepata fedha za mikopo ya muda mrefu na nyingine kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo, ili kuhakikisha tunapiga hatua kwenye sekta ya kilimo," anatamka Waziri Bashe.

Inaendelea Uk 12

## BIASHARA

# Biashara ya kuuza petroli vijijini ilivyo janga linalohatarisha makazi yao wauzaji

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

UNAPOZUNGUMZIA nishati ya mafuta ni pamoja na mahali salama pa utunzaji bila ya kuathiri maisha ya watu, mali zao na eneo zima.

Katika maeneo mengi vijijini baadhi ya makazi yamegeuzwa vituo vya kuuzia mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kutokana na wafanyabiashara wadogo kukosa mitaji ya kujenga vituo vya kuuzia mafuta hayo.

Uamuzi wa wafanyabiashara hao, unaweza kusababisha baadhi ya makazi hayo kuungua moto kutokana na familia kupika vyakula bila ya kuchukua tahadhari na kuhatarisha maisha ya watu na mali zao.

Wafanyabiashara hao, wamekuwa wakisafiri kwenda katika miji mikubwa kununua mafuta hayo na kuyasafirisha usiku na wanapofika vijijini huyahifadhi kwenye makazi na kuyauza reja reja kwenye chupa.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, kuna vituo vingi vya mafuta vinavyofanya kazi usiku, wateja wao wakiwa wafanyabiashara wadogo kutoka vijijini wanaodaiwa hawalipi mapato ya kiserikali.

Kutokana na biashara hizo kuendelea kufanyika katika makazi kinyemela, wananchi wa Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama wameiomba EWURA kuingilia kati ili kudhibiti majanga ya moto yanayoweza kutokea kwenye makazi yao na kusababisha vifo na uharibifu wa mali.

### WANANCHI WAONGEA

Mkazi wa Kata ya Ulowa Halmashauri ya Ushetu, Gabriela Kimaro, anasema wapo hatarini kukumbwa na majanga ya moto kwa kutokana na mafuta hayo kuhifadhiwa kwenye madumu ya lita 20 na mapipa.

Juma Bundala, Mkazi wa Kata ya Segese Halmashauri ya Msalala anasema biashara hizo zimekuwa zikifanyika maeneo ambayo hakuna umeme.

Anasema wafanyabiashara hao wanahifadhi zaidi ya lita 1,000 za mafuta kwenye makazi yao na yanapotokea majanga ya moto mali zao zinateketea. Mkazi wa Mtaa wa Nyasubi Manispaa ya Kahama, Mwasiti Bajora anasema hata mjini kumejengwa vituo vingi vya mafuta jirani na makazi na kuzua hofu miongoni mwao.

### MADIWANI KATA

Doa Limbu, Diwani wa Nyankende Halmashauri ya Ushetu, anathibitisha kuwapo kwa wafanyabiashara hao katika eneo lake kugeuza makazi yao vituo vya kuuzia mafuta na kuhatarisha maisha ya watu na mali zao.

Anasema, wanahifadhi mafuta kwenye mapipa na pikipiki ndani ya makazi yao, wanapika huku kukiwa na joto la moto wanaopikia vyakula ambao unaweza kusababisha moto.

Diwani wa Sabasabini, Emmanuel Makashi, anasema wamekuwa wakikemea biashara hiyo isiendelee kufanyika katika makazi bila mafanikio.

"Uhifadhi wa mafuta haya sio salama wanayachanganya na vyakula, mifugo, vifaa vya usafiri na wanapikia jirani na mafuta mapipa au madumu yanapopata joto yanalipuka na kuleta maafa," anasema na kusisitiza kuwa:

"Tunaendelea kuwaelimisha wananchi kuhifadhi mafuta mbali na makazi kupitia mikutano ya hadhara. "

WAUZAJI VIJIJINI

Wauzaji mafuta hayo vijijini ambao hawakutaka majina ya kutajwa gazetini, wanasema wanafanya biashara hizo katika maeneo hayo kwa sababu hakuna vituo vya mafuta ilhali hawana ajira.

Wanadai wananunua mafuta hayo katika vituo vya mafuta vilivyopo mjini kwa bei elekezi ya serikali na kuuza kwenye chupa lita moja kati ya Sh.3,000 hadi Sh. 3,500.

Wanasema wateja wao wakubwa kuwa ni waendesha bodaboda, wamiliki wa mashine za kusaga nafaka na wachimbaji wadogo wa madini.

Hata hivyo, wanaishauri Serikali kujenga vituo vya kuuzia mafuta katika maeneo ya vijijini ili kudhibiti biashara hiyo haramu.

### MENEJA KANDA YA ZIWA

Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, George Mhina, anakiri kuna baadhi ya wafanyabiashara wadogo vijijini wamegeuza makazi yao vituo vya kuuza mafuta hayo.

Anasema wamekuwa wakifanya msako mara kwa mara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na kuwachukulia hatua za kisheria, ikiwamo kuwatoza faini wafanyabiashara wanaokutwa na hatia.

Kupitia Nipashe anatoa rai kuwataka wafanyabiashara hao kufuata utaratibu wa kuanzisha vituo vya kuuza mafuta hata vyenye pampu moja, ili kukabiliana na hatari ya majanga ya moto.

"Tutaendesha msako katika mikoa ya Kanda ya Ziwa ili kuwabaini wafanyabiashara wote wanaouza mafuta kwenye chupa za maji mbele ya nyumba na maduka yao ya biashara, kwa sababu kufanya hivi ni kwenda kinyume na maelekezo ya EWURA," anasema Mhina.

"Mafuta ni kimiminika hatari ambacho huhifadhiwa kwenye matanki yanayochimbiwa ardhini, lakini wafanyabiashara hawa wadogo wanauza mafuta kwenye chupa za maji kwa kuziweka nje juani hali ambayo inaweza kusababisha mlipuko na mafuta kukosa ubora pindi yanapotumiwa kwenye vyombo vya moto, " anaongeza kusema.

Mhina, anasema mikoa ya Kanda ya Ziwa inaongoza kwa matukio ya nyumba kuungua kwa moto unaosababababishwa na kuhifadhi petroli na dizeli kinyemela kwenye makazi ya watu.

Anasema, matukio hayo ya moto pia yamekuwa yakisababisha upotevu wa mali kutokana na kuteketea, watu kupata ulemavu na wengine kufa kwa kukosa hewa na majeraha.

### VITUO MAFUTA VIJIJINI

Mhina, anasema kuna utaratibu unaowataka wamiliki wa vituo vya mafuta vilivyopo mjini kuhakikisha wanajenga vituo vingine hususani maeneo ya vijijini, ili kudhibiti wimbi la wauzaji mafuta hayo, wasiokuwa na leseni.

Anasema na kwa wale wanaoishi pembezoni mwa barabara hawakatazwi kuanzisha vituo hivyo ili kupambana na biashara hiyo holela.

Mhina anasema, EWURA kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) sasa wana mpango wa kuwakopesha wafanyabiashara hao mikopo nufuu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mafuta vijijijini, ili kukidhi mahitaji ya mafuta kutokana na kuongezeka kwa usafiri wa bodaboda.

Anasema, ili kuomba mkopo huo REA kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mafuta vijijini au pembezoni mwa mji, mfanyabiashara anatakiwa kuwa na mhutasari kikao cha kijiji, mchoro, barua ya mazingira kutoka Baraza la Taifa ya Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) na kibali cha ujenzi kinachotolewa na EWURA kisha kujaza fomu ya REA ya mkopo.

Anaendelea, kusema kuwa vituo vingi vya vya mafuta vilivyojengwa mjini vimekidhi vigezo vya usalama wa mazingira kwa sababu kabla ya kujengwa wamiliki wake wanatakiwa kuwa na hati miliki inayoonyesha eneo sio la makazi, kibali cha mazingira, kibali cha ujenzi kutoka halmashauri, mchoro na kibali kutoka ofisini kwake.

Anasema EWURA inawakaribisha wafanyabiashara wenye nia ya kuwekeza katika biashara ya mafuta ili kuimarisha upatikanaji wa nishati ya huduma ya mafuta vijijini na kukabiliana na uuzaji wa mafuta kiholela na majanga ya moto ambayo yamekuwa yakipoteza maisha ya watu na wengine kupata ulemavu wa kudumu.

## MKUTANO KILIMO AFRIKA WAMUACHIA DK. SAMIA SH. TRILIONI MOJA ZA SEKTA

**INATOKA UK 11**

Anafafanua lengo lililopo ni kuona ifikapo mwaka 2030, sekta ya kilimo ikiwa imepiga hatua katika maeneo mbalimbali nchini, huku akisisitiza wakulima watafanya kilimo cha biashara.

Waziri Bashe anaishukuru serikali kuwekeza fedha nyingi katika sekta yake, kilimo, kwamba inachangia kuipigisha hatua kubwa, ikiwamo kwa wakulima wote kuingia kwenye kilimo chenye tija, kinachotoa ushindani kimataifa.

### MGAWO WA KILICHOPATIKANA

Waziri Bashe anasema pesa zilizopatikana katika mkutano huo, zinaenda kuboresha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, yakiwamo mashamba ya serikali, pia uchimbaji mabwawa, hali inayowezesha kilimo kupiga hatua maradufu, kama ilivyonuia bajeti ya mwaka huu wa fedha.

Anasema katika mkutano huo kama nchi na sekta ya Kilimo, wamefanikiwa kupata fedha, kutoka benki ya Dunia,na safari hii wamepata fedha kwa ajili ya kilimo, kutoka Benki hiyo na wadau wengine ambazo zitakwenda kuboresha katika eneo la umwagiliaji.

Anafafanua zaidi ya kuwa miradi iliyopata



Rais Samia Suluhu Hassan, akijibu maswali wakati wa Mkutano wa Mifumo ya Chakula Barani Afrika, uliomalizika hivi karibuni jijini Dar es Salaam. **PICHA RENATHA MSUNGU.**

ni ile anayoitaja kwa jina Legas Programu za Food Syetem, ambapo miradi ya kinamama na vijana imefanikiwa kupata fedha hizo kwa ajili ya kuendeleza.

"Kama mnakumbuka Rais alizindua rasmi Programu ya vijana ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT). Ilikuwa Machi mwaka huu na vijana hao wameshahitimu mafunzo hayo, wanasubiri kukabidhiwa mashamba yao kwa ajili ya kwenda kuanza kilimo cha uzalishaji," anasema Waziri Bashe.

Anafafanua kwa upande huo wa kilimo cha umwagiliaji, hadi sasa kuna jumla ya hekta 37,000 zitaenda kujengewa mifumo.

Anataja kuwapo programu za kilimo kitaifa, zikiwemo zinazoitwa 'Blog Farm 'za Dogoe Dodoma na Chunya Mbeya. Pia, anataja mradi wa Ikang'asi, Njombe.

Bashe anaitaja kuwa ni miradi mikubwa kitaifa, ambayo inagharamiwa na Benki ya Maendeleo Afrika, huku fedha nyinginezo zitaenda katika kilimo cha mboga na matunda nchini.

"Hizi ni fedha nyingi sana katika kilimo na zinatumika ndani ya miaka mitano," anatamka Bashe, akifafanua, lakini wao sekta ya kilimo, wamepanga kuifanikisha mradi hiyo ndani ya miaka mitatu.

"Katika hilo (fedha) tumefanikiwa, kilichobaki ni utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kilimo hapa nchini," anatamka Bashe.

### SERIKALI ILIVYOJIPANGA

Rais Dk. Samia anafafanua serikali imejipanga kuboresha miundominu hitajika ya Barabara katika mikoa na wilaya, kuhakikisha mazao ya wakulima yanasafirishwa bila ya changamoto yoyote ya kupelekwa sokoni.

Dk. Samia anaahidi, pia wataboresha gati za bandari nchini, ikiwamo katika bandari kuu za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Zanzibar, lengo ni kurahisisha meli za mizigo kuingia na kutoka kirahisi, kwa ajili ya kupakia mazao ya ndani kupeleka nje na kupokea mizigo itokayo nje ya nchi.

Vilevile, anataja kuwa serikali imenunua ndege ya mizigo ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), ambayo nayo itatumika kubeba mazao ya wakulima kusafirisha kwenda nje kwenye soko ilikolengwa.

Ni wiki hii, Rais Dk. Samia amekuwa ziarani mkoani Lindi ambako amezindua ujenzi wa barabara kiwango cha lami, ikigusa wilaya kama za Masasi, Nachingwea, Ruangwa na Liwale na kuzindua Bandari ya Uvuvi, huko Kilwa.

### MNUFAIKA WA MKUTANO

Washiriki wa mkutano, wakulima na wafanya biashara wanakiri kunufaika na mikutano katika hatima ya uendeshaji biashara hiyo, ikiwamo kuongezea bidhaa thamani, kwa ajili ya kuzisafirisha nje ya nchi.

Christopher Magese, anasema wakulima na wafanyabiashara nchini wanapaswa kufanya mageuzi ya kilimo au biashara wanayofanya, baada ya kushiriki mkutano huo wamejifunza vingi kutoka kwa wageni na wenyeji, pia kutoka kwa waliopiga hatua kwenye kilimo.

"Naomba wakulima na wafugaji tubadilike, kilimo ukifanya kwa kufuata kanuni kutoka kwa wataalam utapiga hatua kwa kiasi kikubwa," anasema Magese.

### MAFANIKIO & MATARAJIO

Waziri Bashe anataja mafanikio yanajumuisha, serikali na wizara kwa ujumla kupata fedha za kuboresha miundombinu ya sekta ya kilimo, pia wafanyabiashara wameweza kuingiza fedha nyingi kwa kipindi chote cha mkutano huo kutoka kwa wageni waliofika katika jiji la Dar es Salaam.

Bashe anasema, matarajio makubwa katika sekta ya kilimo ni kuwaona wakulima wanafanya kilimo biashara, ambacho kitawainua kiuchumi na familia zao, pia taifa kwa ujumla.

Dira kuu anaitaja, ni kuhakikisha Afrika inajitegemea katika kilimo na si kusaidiwa ilivyo sasa, hivyo mawaziri hao wameazimia kukutana na kuendeleza kupanga mikakati kwa ajili ya kuinua kilimo barani Afrika.

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Maofisa usafirishaji hawa wapelekwe Rwanda kujifunza!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

MWAKA 2005 nilipata fursa ya kuzuru Rwanda. Nilifikia Kigali, ambako ni mji mkuu wa Taifa hilo lililopitia misukosuko mingi, kubwa likiwa ni la mauaji ya kimbari mwaka 1994.

Nilikwenda wakati ambao nchi ilikuwa inajijenga upya, inapata uponyaji chini ya Rais Paul Kagame. Mimi na wenzangu tulijifunza mengi kuhusu chimbuko la mauaji hayo, madhara na matokeo yake.

Sitaki kurudi huko kuyasimulia, kwa sababu yana machungu mengi, ila nilichojifunza kikubwa ni jinsi Wanyarwanda wakati huo walivyokuwa wanajipanga kujijenga upya.

Nidhamu ilikuwa ya hali ya juu, huku waliohusika na mauaji hayo nao wakifikishwa katika Mahakama Maalum za Gacaca na kupatanishwa na waathiriwa wao, ili kusameheana na kusonga mbele kama Taifa.

Nilishuhudia waziwazi nidhamu ya vyombo vya dola, kwa maana ya wanajeshi na polisi wa nchi hiyo, kokote ulikoenda na kukutana nao walionekana wenye nidhamu na waliopenda kazi yao na kuitekeleza kikamilifu.

Hata madereva walitusimulia, jinsi ilivyo kazi kubwa kukiuka sheria za usalama barabarani, pia ilivyo mwiko kuchafua mazingira hususan jijini Kigali.

Dereva yeyote awe wa gari dogo au kubwa, asingeondoa gari bila yeye na wewe abiria, kufunga mkanda. Kifupi sheria za usalama barabarani zilifuatwa na kuheshimiwa.

Bila shaka hata adhabu kwa mkiukaji ilikuwa nzito. Nimekumbuka haya, kutokana na tukio la hivi karibuni la mchezo wa soka uliofanyika Jumamosi iliyopita, katika uwanja wa Pele jijini Kigali ukikutanisha miamba ya soka ya Tanzania ya Yanga na ile ya Sudan ya Al Merreikh.

Sitaki kurudia matokeo yalikuwaje, kwa sababu kila asomaye hapa anajua nini kilitokea Kigali jioni ya siku hiyo, ambao mamia ya Watanzania walijitokeza kushuhudia mechi hiyo, wakisafri kutoka mikoa mbali mbali ya nchi hadi Kigali.

Kilichonishitua, ni kusikia jinsi baadhi yao walivyousifua mji wa Kigali kwa usalamana nidhamu barabarani, huku baadhi yao wakisema jiji lile ni la kijani kama ilivyo Yanga, bila shaka wakimaanisha uoto.

Sitaki kufika huko, ila wananikumbusha nilichokishuhudia mwaka 2005, kwamba kumbe hakijabadilika na badala yake kimeimarika, kwani mmoja alisema alishangaa kuona jinsi madereva wabodaboda wanavyoheshimu sheria za barabarani.

Alisema alishangaa kuwaona muda wote wamevaa kofia ngumu na wakiheshimu taa za kuongoza magari na vyombo vingine vya moto barabarani, sambamba na kivuko cha pundamilia.

Ni lazima washangae kuona nidhamu hiyo, kwani nchini hicho kitu hakipo asilani. Tanzania baada ya madereva wa bodaboda kubatizwa jina la Maofisa Usafirishaji, hakika hata askari wa usalama barabarani nao wameshikwa upofu dhidi yao.

Si ajabu Tanzania kumshuhudia bodaboda akikatiza alama za pundamilia bila kusubiri waenda kwa miguu wavuke, na kwao taa za barabarani ni sawa tu na miti mingine iliyojiotea pembeni, kwamba haziwahusu kabisa.

Wamekuwa wakifanya hivyo mbele ya trafiki, ambaye anaona ni bora kumsimamisha dereva wa gari atasimama kuliko wa bodaboda asiye na kofia, aliyepakia mshikaki na asiyejali alama zozote za barabarani.

Maofisa Usafirishaji hao wa Tanzania hivi sasa ni wafalme wasioguswa na yeyote na ambao trafiki yuko tayari awapishe wapiti, hata kama wamepakia abiria 20 kuliko kuwakamata, ila bora afe na wa gari.

Wakati maofisa hao wakifanya fujo barabarani huku kudra za Mungu nazo zikiwafuatilia kwa kuwawezesha kuvunjika miguu, kupasuka vichwa na kupoteza maisha kwa ajali, wa magari anasimamishwa kila mita 100 kuulizwa kama wana leseni au hata kutafutiwa kosa ili kutoa kitu kidogo cha kununulia kiwi.

Hayo yanafanyika kwenye bodaboda, huku pia ile amri ya kutupa taka ovyo barabarani ikiendelea, tofauti na jamaa zangu mashabiki wa Yanga walichokishuhudia Kigali, ambako Barabara ni safi kuliko ilivyo Dar es Salaam, achilia mbali mikoani.

Mtu mzima unakaa na kujiuliza, hivi Watanzania tunakosea wapi? Rwanda ambayo huko nyuma ilikuja kujifunza mambo mengi kwetu, leo sisi ndio wa kukimbilia huko kujifunza hata nidhamu ya barabarani na mazingira, kweli?

Ila hili la bodaboda hebu Jeshi la Polisi litoke hadharani liseme tu, kuwa limewashindwa hao maofisa usafirishaji ambao kwao ajali ni sehemu ya maisha.

Kwao marufuku zitolewazo na serikali haziwahusu. Ona wanavyokatiza barabara za mabasi yaendayo kasi licha ya kelele zote hizi! Wapelekwe mafunzo Rwanda basi!

BIASHARA

# Manispaa yabuni maboresho sokoni, huduma mahsusi kwa muuzaji mwenye mtoto mgongoni

**Yasmine Protace**

UANZISHAJI masoko sehemu husika, ni moja ya mafanikio kwa jamii katika kuyatumia kujikwamua kiuchumi, pia serikali inajipatia mapato kupitia masoko hayo.

Kikubwa huwa inatakiwa kuwapo miundombinu rafiki kwa wafanyabiashara, ili waweze kuendesha shughuli zao katika mazingira mazuri.

Ili kuhakikisha biashara zinafanywa katika mazingira mazuri, baadhi ya masoko yameanza kuboresha miundombinu yake, kwa kuweka vyumba maalum, ili waweze kuwanyonyesha watoto wao kwa amani.

Hilo linaonekana katika soko la Manispaa ya Ilala jijini, Dar es Salaam, imekuja na ubunifu unaoyaboresha masoko yake, ikiwamo kujenga vyumba vya watoto kunyonyeshewa na vyumba vya watoto kupatiwa elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa jijini Dar es Salaam, Jomaary Satura, anaiambia Nipashe kwamba lengo la manispaa yake ni kuboresha ustawi wa maisha ya wananchi, kwa kuwaboreshea maeneo ya kufanyia biashara kinamama wanaonyonyesha.

"Katika masoko mengi wafanyabiashara wanawake,wengi wao hufika katika biashara na watoto wadogo,ambao wapo katika umri wa kunyonya," anatamka mkurugenzi.

Hadi sasa, masoko mengi wafanyabiashara wake ni wanawake, ambao wanapoboreshewa maeneo yao ya biashara, kitafsiri anakuwa kasadiwa kuinuka kiuchumi.

Anaongeza kwamba kuna wafanyabiashara wasio na watu wa kuwaachia watoto, hivyo watoto wanapotoka shule huenda sokoni kuwasubiri wazazi wao, ili jioni warudi nao nyumbani.

Anaitaja changamoto kwao, mtoto kutoka shule kwenda katika biashara sokoni kwa mama yake kumsuburi, hapo inakuwa hatari kwa mtoto huyo kufanyiwa vitendo vya ukatili.

"Baada ya kubaini changamoto hizo, tumeona ni vyema kuwapo na vyumba, mtoto akitoka shule anafika sokoni aendelee kupata elimu ili asifanyiwe ukatili au kujiingiza katika yasiyofaa na wale ambao umri wao ni wa kunyonya, nao wataendelea kupewa huduma hizo,wakiwa katika vyumba,"anasema.



Shughuli za kilimo, zikiendelea sokoni Ilala, Dar es Salaam. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

Anaongeza kuwa hadi sasa utaratibu unaandaliwa ili wawachukue na watoto wa mitaani, ili nao wapate elimu katika vyumba hivyo.

Ofisa wa Maendeleo wa Manispaa ya Ilala, Fransisca Makoye, anasema maofisa maendeleo walienda katika masoko ya Ilala na kuchukua takwimu kupata picha ya uhalisia.

Ni takwimu zinazotajwa zitawasaidia namna ya kuwaandalia vyumba hivyo kwa ajili ya watoto ambao mama zao hufanya biashara katika masoko.

Anaongeza, kuwa maeneo ya kuwalea watoto yataandaliwa huku wao wakiendelea kufanya biashara zao. Hapo Fransisca anafafanua:

"Masoko yote ya Ilala yanaboreshwa, kutakuwa na eneo la kunyonyeshea watoto, ikiwamo na eneo la kuwalea watoto pale wanapotoka shule kuja sokoni kuwasubiri wazazi wao," anasema.

> **"Masoko yote ya Ilala yanaboreshwa, kutakuwa na eneo la kunyonyeshea watoto, ikiwamo na eneo la kuwalea watoto pale wanapotoka shule kuja sokoni kuwasubiri wazazi wao," anasema.**

Anaongeza kuwa, takwimu zimeshachukuliwa kujua idadi ya watoto wanaokuja na wazazi wao katika biashara, ili ujenzi uweze kuendana na idadi yao.

Ofisa huyo anasema, baada ya kukamilika majengo hayo wataandaa gharama zitakazokuwa rafiki, ili zitumike na watoto watakuwa wanapatiwa elimu katika vyumba hivyo, wazazi nao watachangia gharama kidogo.

Hance Obote, Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa, Saranga, jijini Dar es Salaam, anasema matukio ya ukatili yanafanywa zaidi kwa watoto wanaozurura katika masoko.

Anaahidi vyumba vikiandaliwa vya kuwalea watoto, vitazingatia watoto kupatiwa huduma za elimu ma nyiginezo, akinena: "Kuna watoto ambao mtoto mwenye umri wa kuanzia miaka tisa, mpaka miaka minne.

"Huyo akiwa sokoni na mama yake haina shida, lakini uangalizi unatakiwa kuwepo ili asijifunze mambo ambayo baadaye yanaweza kuchangia hata makuzi yake kuwa mabaya," anasema. Anaongeza, wapo watoto wenye umri miaka minne hadi mitano, haoo hawatakiwi sokoni, bali wawepo shule wakipata elimu.

Anasema, baadhi ya watoto walio na umri wa kwenda shule, huwa hawaendi, wanakuwa katika biashara za sokoni na mama zao.

" Kutokana na watoto kutoenda shule na kuzurura katika biashara za wazazi wao sokoni wanakuwa wakifanyiwa ukatili wa kijinsia," anaeleza.

Hance anasema, baadhi ya watoto wamekuwa wakifanyiwa ukatili kutokana na kuzagaa kwao sokoni, huku mama zao wakiwa 'bize' na biashara zao.

Anataja muhimu sokoni ni uwekezaji kwa wanawake, hivyo kunatakiwa kuwapo vyumba vya kulea watoto ili wahakikishiwe usalama.

Ofisa huyo anaongeza kuwa serikali inapotoa mikopo kwa wanawake, inapaswa kuzingatia mikopo hiyo, iwe mahsusi ya biashara.

Consolata Phacras, ni mkurugenzi katika masuala ya usaidizi wa kisheria katika masoko 10 ya Ilala jijini Dar es Salaam, anasema hali duni ya maisha inawafanya wafanyabiashara wanawake masokoni kwenda na watoto wao katika biashara.

Anafafanua kwamba, kwa mama sokoni anakuwa kambeba mwanawe, huku akipika chakula cha biashara na kuna wanawake wengine sokoni hufanya biashara za matunda au mboga wakiwa na watoto mgongoni.

"Kinamama wengi ukiwahoji sababu za kuja na watoto sokoni,wanasema hawana uwezo wa kuajiri watu wa kukaa na watoto wao," anasema Consolatha.

Anasema ili wanawake wa sokoni walio na watoto ambao wanakuja nao katika biashara kufanya biashara kwa utulivu, kunatakiwa kuwapo utaratibu wa kuwekwa maeneo ya kuwalea.





Wakazi wa kijiji cha Magungu, wilayani Chemba, mkoani Dodoma, wakiswaga punda waliowabebesha madumu ya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Asasi zajadili utekelezaji mpango SADC

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASASI za kiraia zimekutana jijini Dodoma kujadili utekelezaji wa mpango mkakati wa Jumuiya na Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambao unazitaka nchi wanachama kuwa na uchumi wa kati wa viwanda na amani ili kuwa na maendeleo endelevu ifikapo 2050.

Mkurugenzi wa Shirika la ActionAid Tanzania, Bavon Christopher, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye kikao cha siku tatu cha kujadili Tanzania ilivyofanikiwa kuutumia mpango mkakati huo kwenye mipango yake ya ndani.

Christopher alisema lengo la kikao hicho ni kutathimini ni kwa namna gani Tanzania imeuweka mpango mkakati huo kwenye mipango yake ya ndani.

"Mpango mkakati huu ni wa miaka 10 kuanzia 2020 hadi 2030 ambao umejikita katika kuboresha viwanda, kilimo, miundombinu, haki za binadamu, mapambano dhidi ya mabadiliko tabianchi na mambo mengine," alisema.

Alisema kikao hicho pia kimejumuisha wadau kutoka asasi mbalimbali za kiraia na wawakilishi wa serikali kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na wabunge wa SADC.

"Maono ya SADC ni kuona nchi wanachama zinakuwa na uchumi wa kati wa viwanda na amani inadumishwa ili kuwa na maendeleo endelevu kwa wananchi ifikapo mwaka 2050. Lengo la kukutana hapa ni kuona ni kwa jinsi gani yale ambayo tulijipangia kuyatekeleza sisi kama asasi tumeyafanikisha.

"Lakini pia serikali yetu imetekeleza kwa kiasi gani kuufanya mpango mkakati huu wa SADC kuwa sehemu ya mipango yake ya ndani ambayo itatekelezwa lakini pia kazi yetu sisi ni kuisimamaia serikali, kuishauri na kutoa msaada wowote inaouhitaji ili kufanikisha utekelezaji wake," alisema Christopher.

Pia alisema kikao hicho ni mwendelezo wa vikao vya awali ambavyo vilitumika kwa ajili ya asasi za kirai pamoja na serikali kujiwekea malengo ya utekelezaji wa mpango mkakati huo.

"Kikao cha kwanza tulikaa mwaka 2021, cha pili 2022 na hiki leo ni cha tatu. Tunaangalia ni kwa kiasi gani tumetekeleza lakini ni mambo gani yanapaswa kufanywa kuanzia leo hii hadi hapo tutakapokutana tena Septemba mwakani. Vivyo hivyo, kwa serikali pia kueleza nini imefanya na nini watafanya kuanzia leo hii hadi mwakani tutakapokutana tena," alisema

Hata hivyo, aliipongeza serikali ya Tanzania kwa namna ambavyo inaendelea kushiriki katika SADC, hali ambayo itasaidia taifa kupiga hatua kiuchumi.

"Niwapongeze sana viongozi waliotangulia akiwemo Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, ambaye aliona kuna umuhimu wa sisi kama taifa kushirikiana na mataifa mengine katika jumuiya kwani sisi Afrika hatuwezi kupiga hatua kama hatutakuwa wamoja. Umoja ndiyo siri ya mafanikio yetu.

"Leo hii tunapoondoa vikwazo katika mataifa mengine, tunaruhusu usafirishaji wa bidhaa zetu kutoka nje na zingine kuingia ili kuimarisha uchumi wetu na bara letu kwa ujumla," alisema.

Daines Mtei kutoa Wizara ya Kilimo, alisema kikao hicho ni fursa kwa serikali pamoja na Asasi za kiraia nchini kuelezea mambo mbalimbali ambayo yanahusu jumuiya ya SADC hasa utekelezaji wa mpango mkakati wa kuziwezesha nchi za Afrika kuwa na uchumi wa kati wa viwanda na amani.

# Kiwanda chapongezwa kuheshimu sheria kazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amekipongeza kiwanda cha mbolea cha ITRACOM cha jijini Dodoma kwa kuzingatia sheria za kazi.

Prof. Ndalichako aliyasema hayo juzi alipofanya ziara katika kiwanda hicho kwa lengo la kukagua utekelezaji wa sheria za kazi na kuwataka wawekezaji nchini kuiga mfano wa kiwanda hicho.

Alisema utekelezaji wa sheria za kazi ambao umefanywa na kiwanda hicho ni pamoja na kuwapa mikataba wafanyakazi, usalama na afya mahali pa kazi na kuwasilisha michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kwa wakati.

Aidha, Prof. Ndalichako alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya wawekezaji nchini.

"Uwekezaji wa kiwanda hichi cha mbolea umezalisha ajira za awali 1,198 na kitakapokamilika ajira za moja kwa moja 3500 zitazalishwa na ambazo sio za moja kwa moja zitazalishwa ajira 8,000," alisema.

Pia alipongeza kiwanda hicho kwa kutoa fursa kwa wafugaji kuuza mbolea yao aina ya samadi ambayo inatumiwa na kiwanda hicho kama malighafi ya uzalishaji wa mbolea.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, aliahidi kuendelea kuimarisha mazingira wezeshi kwa wawekezaji ili uwekezaji wa kiwanda hicho ukamilike kwa wakati na kuwa na tija kwa wananchi. Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Kiwanda hicho, Kimaramuziro Nkurikiye, aliishukuru serikali kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwenye ujenzi wa kiwanda hicho na kutatua kero zilizokuwa zinawakabili ikiwemo maji, umeme na barabara.

# Balozi asisitiza ushirikiano Tanzania, Indonesia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BALOZI wa Indonesia nchini Tanzania, Tri Yogo Jatmiko, amesisitiza kuendeleza ushirikiano na Tanzania katika kutangaza mwelekeo mpya wa Wizara ya Madini unaofahamika kama Vision 2030 Madini ni Maisha na Utajiri, ili kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo katika sekta hiyo nchini.

Balozi Jatmiko, alisema hayo jana jijini hapa baada ya mazungumzo mafupi na Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Kheri Mahimbali, katika kikao kilicholenga kujenga uhusiano baina ya nchi hizo katika uchimbaji madini

"Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali mbalimbali za madini ambazo ni muhimu na zinahitajika duniani.

Kupitia dira hiyo, sekta ya madini inakwenda kutangaza nchini Indonesia na kueleza wawekezaji fursa mbalimbali zilizopo," alisema Jatmiko.

Pia alisema kutokana na mahitaji makubwa ya matumizi ya madini husussan magari ya umeme katika nchi hiyo, serikali ya Indonesia itaweka vipaumbele katika matumizi ya madini kutoka nchini Tanzania ili kukidhi mahitaji yao katika matumizi mbalimbali ya vifaa vya umeme.

Katika hatua nyingine, alimpongeza Waziri wa Madini, Antony Mavunde, kwa kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuongoza wizara hiyo.

Alisema nchi hiyo itatoa ushirikiano wa kutosha nchini ili kuvutia uwekezaji katika sekta ya madini.

Katibu Mkuu Mahimbali alisisitiza kutoa ushirikiano katika kuwajengea uwezo wataalam mbalimbali wa wizara na taasisi katika maeneo ambayo yatahitajika ikiwamo mafunzo ya uongezaji thamani madini na mafunzo maalum kwa wakufunzi wachache ambao watakuwa walimu katika kutoa mafunzo maeneo muhimu.

Pia alieleza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizoko katika sekta ya madini ikiwamo ushirikiano katika uchimbaji wa dhahabu na madini ya kimkakati.

"Tunahitaji ushirikiano katika maeneo ya uchimbaji wa madini hayo kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na sisi serikali tutatoa ushirikiano ili uchimbaji wa madini hayo ufanyike hapa nchini," alisema.

Pia aliwakaribisha kushiriki katika Jukwaa la Kimataifa la Uwekezaji katika Sekta ya Madini linalotarajiwa kufanyika Oktoba 25 na 26, mwaka huu, ambalo litatangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo nchini.





Mlezi wa Jukwaa la kiuchumi la waandishi wa habari wa mkoa wa Mbeya (MJEF), Ndele Mwaselela akizungumza na wanahabari na baadhi ya vijana wakati wa chakula cha jioni alichowaandalia juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wataka ubora miundombinu Ziwa Nyasa kuepusha maafa

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WANANCHI wanaotumia usafiri wa meli ndani ya Ziwa Nyasa, wameiomba serikali kuboresha miundombinu ya bandari ndogo ili kuepusha maafa wakati ziwa linapokuwa limechafuka.

Wakizungumza kwenye kikao cha kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Bandari nchini ambayo kwa bandari za Ziwa Nyasa yamefanyika wilayani Kyela, baadhi ya wananchi walisema ziwa hilo lina bandari nyingi lakini zenye miundombinu inayofaa ni chache.

Zacharia Mbilinyi, mkazi wa Kyela, alisema kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa kuna bandari nyingi ambazo zinapitiwa na meli za abiria lakini baadhi hazina miundombinu rafiki kwa meli hizo kutia nanga. Alisema hali hiyo inahatarisha usalama wa abiria wanaokwenda kupanda meli hizo.

"Kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa tuna bandari 15 lakini ukiangalia zenye miundombinu rafiki ni bandari tano tu. Tunaomba serikali iboreshe miundombinu kwenye bandari hizi ili iwe rafiki kwa watumiaji," alisema Mbilinyi.

Alisema endapo bandari zote zitaboreshwa kwa kujengewa miundombinu rafiki, itasaidia hata abiria wanaotumia meli hizo kuongezeka na hivyo serikali licha ya kutoa huduma nzuri kwa wananchi wake pia itaongeza mapato.

Lupakisyo Mbilinyi ambaye ni Mkazi wa Matema, alisema katika uboreshaji huo wa miundombinu ya bandari, yanahitajika pia majengo ya abiria kukaa wakati wakisubiri usafiri.

Alisema kwa sasa katika baadhi ya bandari za Ziwa Nyasa ikitokea meli imechelewa au kuahirisha safari, abiria wanapata usumbufu kwa kukosa mahali pa kusubiri na wengine wanalazimika kuondoka bandarini na kwenda maeneo ya Jirani, nje ya bandari, kupumzika wakati wakisubiri usafiri wa meli.

"Inapotokea Mamlaka ya Hali ya Hewa wakatangaza kuwa kutakuwa na hali mbaya ziwani hata kusababisha meli ikaahirisha safari kwa muda, abiria wanapata shida kwa kuwa hawana pa kukaa. Tunaomba iwekwe miundombinu ya kuwezesha wananchi kukaa bandarini hapo kusubiri hali ya hewa itulie ili waendelee na safari," alisema.

Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Manga Gasaya, alisema serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) tayari imeshaliona tatizo hilo la miundombinu na tayari imeanza kuchukua hatua.

Alisema baada ya kuona tatizo hilo, ilitoa zabuni kwa mkandarasi aliyefanya tathimini na upembuzi yakinifu wa hali za bandari zote za Ziwa Nyasa akiainisha mpaka gharama za ujenzi wa miundombinu kwa kila bandari.

Gasaya alisema kazi hiyo ilishamalizika na ripoti ilishakabidhiwa serikalini na Rais Dk. Samia Suluhu Hassani akaelekeza TPA kuifanyia kazi ripoti hiyo.

Alisema kwa kuanzia katika mwaka huu wa fedha, serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 70 kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mbambabay iliyoko Mbinga mkoani Ruvuma kama mwanzo wa utekelezaji wa ripoti hiyo.

# Watumishi wafundishwa mfumo mpya wa ununuzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, imeanza kutoa mafunzo kwa watumishi wake kuhusu matumizi ya mfumo mpya wa ununuzi wa umma wa kielektroniki (NEST) ambao unalenga kuboresha ununuzi wa vifaa mbalimbali.

Mafunzo hayo yalianza kutolewa juzi kwa watumishi wa kada mbalimbali wakiwamo wa idara za ununuzi, fedha na mipango ambao ndio wanaohusika zaidi na masuala hayo.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Kaimu Mkuu wa Idara ya Ugavi na Ununuzi wa hospitali hiyo, Denis Mtasiwa, alisema uongozi wa hospitali uliratibu mafunzo hayo ili watumishi waufahamu na wautumie kwa lengo la kuboresha huduma.

Mfumo huo, alisema ni mpya, hivyo ili watumiaji wautumie vizuri ni lazima wapatiwe mafunzo ili kutumia kwa ufanisi na kubaini faida zake.

"Mfumo wa NEST unatumia teknolojia ya kisasa ya mtandao na unaruhusu watumishi kufanya ununuzi kwa njia ya mitandao. Hii inamaanisha kuwa ununuzi unaweza kufanyika kwa haraka na kwa uwazi zaidi," alisema Mtasiwa.

Alisema serikali imewekeza kwenye mfumo huo mpya ili usaidie kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kuhakikisha ununuzi unafanyika kwa uwazi na kwa kuzingatia sheria za nchi.

Alisema baada ya kukamilisha mafunzo hayo kwa kundi la kwanza watafuata makundi ya watumishi wengine ili kuhakikisha watumishi wote wa hospitali wanaufahamu na wanautumia kwa ufasaha.

# Wafanyabiashara mbao wadaiwa kuuza risiti feki

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

MENEJA wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Njombe, Specioza Owure, amesema wafanyabiashara wa mbao mkoani hapa wanaongoza kwa kuuza risiti mitaani, hivyo kuikosesha serikali mapato.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kwenye uzinduzi wa kampeni ya TUWAJIBIKE mkoani hapa, yenye lengo la kuhamasisha walipakodi wanapouza bidhaa zao au wanapotoa huduma, watoe risiti za kielektroniki (EFD) ambazo ni sahihi.

Owure alisema baada ya kubaini hilo, walianzisha kampeni iliyofanyika hivi karibuni na kuwanasa wafanyabiashara wa mbao na magari matano na wote wamepata adhabu stahiki.

"Pia tumefanikiwa kunasa mashine mbili ambazo kazi yake ni kuuza risiti na si kufanya biashara ya mbao na mtu kama huyo si kwamba analipa faini kwa sababu anahujumu uchumi. Watanzania tuko milioni 60 lakini anapomuuzia mtu risiti labda mtu amenunua bidhaa ya Sh. milioni 15 labda akapewa Sh. 300,000 akatoa risiti ya Sh. milioni 15 au ya milioni 10 tayari anahujumu uchumi," alisema Owure.

Alisema katika kampeni hiyo wataendelea kuelimisha wafanyabiashara na wananchi juu ya umuhimu wa kudai risiti na kutoa risiti kwa sababu wote wako kwenye kundi la kupata adhabu.

"Adhabu kwa asiyetoa risiti kwa sasa imepunguzwa. Kama unavyojua serikali ni sikivu na mwanzoni ilikuwa Sh. milioni tatu hadi Sh. milioni 4.5 lakini kuanzia Julai, mwaka huu, imebadilika na kuwa Sh. milioni 1.5 au asilimia 20 ya mauzo uliyofanya. Kwa yule ambaye hadai risiti, awali ilikuwa Sh. 30,000 mpaka Sh. milioni 1.5 na nusu lakini kwa sasa hivi ni Sh. 30,000 au asilimia 20 ya kodi iliyokuwapo. Kwa hiyo wote wana adhabu lakini pia kuna kifungo cha miaka mitatu jela au unaweza kupingwa vyote faini na kufungo juu," alisema Owure. Meneja Msaidizi wa Mkoa (Ukaguzi) Sylvester Nzali, alisema kampeni hiyo ni endelevu kwa sababu wanataka kuhamasisha, kuelimisha matumizi sahihi ya EFD.

Naye Meneja Msaidizi Huduma kwa Mlipakodi, Beatrice Kahoho, alisema changamoto kubwa kwa wafanyabiashara ni wakati wa makadirio kwa sababu wanakuwa hawana taarifa sahihi, hivyo kulazimika kuanza kuwahoji upya.

Mfanyabiashara wa mjini Njombe, Evaristo Tave, alisema serikali kupitia TRA, imeanzisha kampeni kwa ajili ya watu kulipa mapato halali na kwa uaminifu.

"Lakini jambo la msingi tunaishauri serikali inapopokea mapato yetu kwa uaminifu basi fedha hii iende mahali husika. Lakini pia kodi tunakadiriwa badala la kukaa mezani kukubaliana," alisema Tave.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara katika Halmashauri ya Mji Njombe, Eliud Pangamawe, alisema kampeni hiyo ni nzuri kwa sababu inahamasisha wafanyabiashara kutoa risiti ili wachukue kodi ambayo ni kwa faida ya taifa zima.





# SMZ yashauriwa kuvunja mkataba ukodishaji bandari Malindi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeshauriwa kuvunja mkataba wa ukodishwaji wa Bandari ya Malindi kwa Kampuni ya Afrika Global Logistics (AGL) ya nchini Ufaransa kama itashindwa kurejesha tozo ya zamani kwa wafanyabiashara bandarini hapo.

Ushauri huo umetolewa na Naibu Katibu Uenezi na Mawasiliano ya Umma wa Chama cha ACT Wazalendo, Salum Bimani wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya wafanyabiashara kugoma kutoa mizigo bandarini wakipinga viwango vikubwa vya tozo ya ushuru tangu kampuni hiyo ianze kazi Septemba 18, mwaka huu.

"Ikiwa hatua hizo zitashindikana, tunataka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk Mwinyi kuvunja mkataba na Kampuni ya AGL na kurudisha uendeshaji wa Bandari ya Malindi kwa Shirika la Bandari la Zanzibar, " alisema.

Alisema kabla ya kufikia hatua hiyo ACT kinaitaka Serikali kuitisha kikao na wadau wa usafirishaji na uingizaji wa mizigo bandarini hapo, wafanyabiashara na AGL kutafuta ufumbuzi wa matatizo yaliyojitokeza baada ya kuanza kutumika tozo mpya za ushuru.

"Tunaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk Mwinyi mara moja kusitisha bei mpya za utoaji na upakuzi wa mizigo na uingizwaji wa gari bandarini zilizotangazwa na Kampuni ya AGL kwa sababu zinavuruga sekta ya biashara na kuongeza mfumuko wa bei Zanzibar," alisema.

Alisema wananchi wa Zanzibar hususani wafanyabiashara wanategemea bandari hiyo kupakia na kupakua bidhaa zao, hivyo hawatapenda kuona uchumi wa Zanzibar unayumba kwa manufaa ya watu wachache. Bimani alisema ni jambo la kusikitisha ukodishwaji wa bandari hiyo haukufanyika kwa uwazi na zabuni ya ukodishwaji haikutangazwa.

Alisema kitendo cha zabuni hiyo kutotangazwa hadharani ni kinyume na sheria ya zabuni na ushindani zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

"Je ni lini zabuni ya ubinafsishwaji wa Bandari ya Zanzibar ilitangazwa na kampuni zipi nyingine zilizoomba, ni utaratibu upi na vigezo vipi vilitumika mpaka kufikia kupelekea kupewa AGL ya Ufaransa uendeshaji wa Bandari ya Malindi?"alihoji.

Alisema kama lengo lilikuwa kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za urasimu, iweje baada ya AGL kukabidhiwa uendeshaji iongeze gharama za utoaji na upakuaji wa mizigo kwa zaidi ya asilimia 200 wakati hawajawekeza vifaa.

Alisema kama serikali ilikuwa na malengo ya kubinafsisha bandari hiyo kwa nini ilitumia Shilingi bilioni 16.5 kununua vifaa vya kisasa vya upakiaji na upakuaji wa mizigo siku chache kabla yakukabidhi wawekezaji hao.

Hata hivyo, alisema inasikitisha mradi huo umefanyika kwa njia za siri licha ya wanasiasa na wanaharakati kupinga uwekezaji huo, lakini bado Serikali iliendelea na msimamo wake wa kubinafsisha bandari hiyo.

Bimani aliendelea kusema kuwa ukodishwaji wa bandari hiyo haukuwa na nia njema bali kilikuwa ni kitendo cha kifisadi cha watu wachache kujilimbikizia mali kupitia mgongo wa Wazanzibari wanyonge.

Akizungumzia tozo holo, Ofisa Uhusiano wa Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) , Hassan Amour amesema viwango hivyo vya tozo siyo vipya kwa kwani vilikuwepo tangu zamani, lakini vilikuwa havitumiki ili kuwapa nafuu wafanyabiashara na wananchi.

"Tozo hizi sio mpya zipo kabla ya kuja muwekezaji huyu wa Ufaransa lakini zilikuwa hazitumiki, sasa walipokuja wawekezaji hawa walitaka wapewe nyaraka zote za uendeshaji wa bandari, ikiwemo viwango vya tozo kabla ya kuanza kuzitumia, " alisema.

Hatua hiyo ya AGL kuongeza tozo siku moja baada ya kukabidhiwa uendeshaji bandari hiyo, kumesababisha kuendelea kwa mgomo wa ushushaji na upakiaji ya mizigo ambayo inasafirishwa kati ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa majahazi, ikiwemo vyakula vya nafaka, viungo na matunda.



Naibu Katibu wa Uenezi na Mawasiliano ya Umma wa Chama cha ACT- Wazalendo, Salum Bimani akizungumza na waandishi wa habari, jijini Zanzibar jana, kuhusu mgomo uliojitokeza wa kutoa na kupakia mizigo katika bandari ya Malindi tangu kampuni ya AGL kukabidhiwa uendeshaji Septemba 18 mwaka huu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# TEHAMA kuitangaza Zanzibar duniani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR inatarajiwa kuwa kitovu cha uwekezaji katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) baada ya kampuni zaidi ya 50 kuonyesha nia ya kufungua ofisi zake visiwani hapa na kujulikana Duniani.

Hayo yalibainika jana wakati wa ufunguzi wa ofisi za Kampuni ya Airpay visiwani hapa.

Hatua hiyo itasaidia kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wananchi kupitia mifumo ya malipo kwa njia ya kidijitali.

Akizungumza wakati wa hafla ya ufunguzi wa ofisi hiyo iliyopo Mlandege mjini Unguja, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji, Mudrick Ramadhan Soraga, alisema itaifanya Zanzibar kuwa kitovu cha uwekezaji wa mifumo ya TEHAMA na kujulikana Duniani.

"Airpay imetufungulia milango ni imani yangu kuwa makampuni mengine mengi yakishaona nao watakuja Zanzibar," alisema Soraga.

Alisema hadi sasa kuna kampuni tatu zinazojihusisha na shughuli za TEHAMA ikiwemo ya Airpay na nyingine 50 zinakamilisha taratibu ili kufanikisha kuweka makao makuu yake kuwa Zanzibar.

Alisema Serikali itaendelea kutoa ushirikiano wa kampuni hiyo ili kuleta mageuzi makubwa ya TEHAMA si tu kwa wajasiriamali wadogo bali hata taasisi za benki kwa kuwa ndiyo wanufaika wakubwa wa teknolojia hiyo.

Alisema changamoto kubwa inayoikabili Zanzibar ni zaidi ya asilimia 70 ya wajasiriamali kutotambulika katika mifumo rasmi.

"Ukitambulika kuna faida nyingi ikiwemo kupata mikopo na mafunzo na kuchangia kulipa kodi, sasa tunataka hadi wale wauza madafu kuwatambua katika mifumo rasmi," alisema.

Waziri huyo alisema kampuni hiyo ni ya kwanza kuweka makao makuu Zanzibar na ina jopo la wataalamu kutoka India ambao watakuwepo Zanzibar kufanya shughuli zao.

Mwanzilishi wa Airpay, Kunal Jhunjhunwala, alisema Zanzibar ni mdau sahihi wa kushirikiana naye kurasimisha mifumo ya kidijitali na kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwa kutochelewa kufanya maamuzi ya kuridhia.

Alisema wamevutiwa na mtazamo wao wa kuifanya Zanzibar kuwa makao makuu ya huduma hizo kwa Afrika na kujenga uchumi usiotegemea mzunguko wa fedha taslimu.

Makamu wa Rais na Meneja Mkakati wa kampuni hiyo, Mihayo Wilmore, alisema itawasaidia wajasiriamali wadogo ili kutambuliwa katika mifumo ya teknolojia ya TEHAMA na kuwarahisishia kuhamisha fedha.

Meneja Uchumi wa Benki Kuu Tanzania (BoT) Ofisi ya Zanzibar, Moto Ng'wingande, alisema wametoa leseni kwa kampuni hiyo ya uendeshaji wa shughuli zake visiwani humo kutokana na uwezo wa vifaa vya uendeshaji wa teknolojia hiyo.

## Wajasiriamali washindwa kujisajili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAIMU Mkurugenzi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BRPA) Rashid Masoud Othman, amesema wajasiriamali wengi visiwani Zanzibar wanashindwa kutumia fursa zilizopo kusajili mali bunifu kwa ajili ya kupata ulinzi kisheria.

Othmani alisema hali hiyo imesababisha ubunifu huo kuchukuliwa na watu wengine.

Aliyasema hayo wakati akifungua semina ya kutoa elimu kuhusu urasimishaji wa kazi za mali bunifu na biashara za wajasiriamali visiwani hapa.

Alisema lengo la kutoa mafunzo hayo ni baada ya kubaini kuwa bado wajasiriamali hao hawajaona umuhimu wa ubunifu.

Alisema mafunzo hayo yatawajengea wajasiriamali hao uelewa wa kurasimisha kazi za ubunifu na biashara kwa maendeleo ya nchi.

Alisema utekelezaji wa mkakati wa matumizi ya mali bunifu utasaidia kuinua harakati za maendeleo ya kiuchumi kama zilivyo nchi nyingine duniani.

Alisema Serikali imeweka sheria, kanuni, miongozo na mazingira bora ya ufanyaji wa biashara nchini.

Kaimu huyo alisema mali bunifu kama vile alama za biashara, uvumbuzi ni muhimu katika kukua kwa maendeleo ya kiuchumi.

Alisema Zanzibar kama nchi nyingine inafahamu umuhimu wa nafasi ya mali ubunifu katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi.

"Sekta hii ina nafasi kubwa katika kukuza ubunifu wa uvumbuzi zaidi katika uwekezaji wa kufanya utafiti na maendeleo," alisema.

Alilitaja eneo jingine muhimu katika kukuza biashara nchini kuwa ni kurasimisha biashara hizo na kusaidia jamii kufanya biashara zao, kujiletea maendeleo na kusaidia upatikanaji wa bidhaa bora zenye viwango.

Salum Rehani kutoka Taasisi ya Wakulima wa Mboga na Matunda, alisema lengo lao ni kuwajengea uwezo wajasiriamali wa Zanzibar ili kuzalisha bidhaa bora na kufikisha katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Alisema kuna bunifu ambazo zinatengenezwa katika biashara ili kufikia masoko zaidi kwa ubora na wingi zinahitaji kusajiliwa kama bidhaa bunifu, lakini wajasiriamali ni waoga.

Wajasiriamali walioshiriki katika mafunzo hayo waliipongeza Serikali kupitia BRPA wakisema yatawasaidia kuwa wabunifu zaidi na kulindwa kisheria.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Rukia Nahoda Juma, alisema kwa sasa Zanzibar ubunifu umepungua hasa kwa vijana, hivyo mafunzo hayo yatawawezesha kusimamia kazi zao wanazobuni na kupata usajili wa hatimiliki.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ANATAFUTWA



**TUMAINI MUSHI** anatafutwa na ndugu zake baada ya kutoweka akiwa kazini Agosti 31 2023 eneo la Gerezani, Kariakoo Dar Es Salaam. Kwa yeyote atakaemuona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apiga simu namba **0754816769/0782309393.** POLISI TAARIFA: **MSZ/RB/5503/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GRAYSON T MAKWINJE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0960/0264** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BENJAMIN WILLIAM MKAPA HIGH SCHOOL** mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/388630/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FELIX JOSEPH MANENO,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SEMI TRAILER (SCANIA)** Yenye no za Usajili **T 505 CGK,** CHASISS **NO 4494644,** ENGINE **NO 6194095,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo Chochote cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/DOD/DOD/3462/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI NA LESENI YA UDEREVA

**MASANJA KASUKA SUNDAY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba **T.623 BQN** na leseni ya udereva yenye namba **4006487917.** Kwa yeyote atakaevioana atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DSM/PHQ/RB/8216857/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FELIX JOSEPH MANENO,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TIPA (TATA)** Yenye no za Usajili **T 405 DGD,** CHASISS MAT **396522E2R08718,** ENGINE NO **B591602041G63387282** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo Chochote cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/DOD/DOD/3469/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya BAGAMOYO**
**Kituo cha KEREGE**
**Mkoa PWANI**

**Shauri la madai/Ndoa Na.........5.../2013**

**Jina la mdai....................................................VERONICA MLAY**

**Jina la mdaiwa...................................CHAMI HUSSEIN MZIMBA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa : CHAMI HUSSEIN MZIMBA**
**KEREGE, BAGAMOYO**

**Kwa kuwa Mdai/wadai ameleta /wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai)**
**KUKAZA HUKUMU**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 29 Mwezi 9 Mwaka 2023 saa 3:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahamkama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 19 mwezi 9 mwaka 2023

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA DODOMA**

**SHAURI A ARDHI NA. 2/2023**

**DEDEA MABWAYI.......................................... MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MASHAKA NGOSI............................................ MJIBU MAOMBI**

**KWA: MASHAKA NGOSI**

**POPOTE PALE ULIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA ARDHI NA. 2/2023 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA**; Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama Kuu Tanzania, kanda ya Dodoma, mbele ya Mhe Jaji F. R. Khalfan, wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma, saa mbili na nusu (8:30) asubuhi siku ya ijumaa tarehe 22/09/2023.
**HIVYO BASI;** Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
**NA ENDAPO;** hautafika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.
**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 8 Mwezi wa September, 2023

Kny: **NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DODOMA**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 108 of 2023**

**In the Matter of the Estate of the LATE PIUS DAUD SEIPH of Buigiri Chamwino within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by SAID JOSEPH BATANO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 04 day of 10........................ 2023
**Dated at Dodoma this 20 day of September...........2023**

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE I/C
DODOMA DISTRICT

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAYMOND RAPHAEL MASSAE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **LANDCRUISER** yenye jina la umiliki **HUMAN OUTREACH TANZANIA** yenye usajili namba **T746 AME.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/ARU/2492/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER JOSEPH MUSHI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina **FIAT TORINO** yenye usajili nmaba: **T 730 ALX.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/ARU/2749/2023**

---

**MAHAKAMA YA WILAYA SINGIDA**
**MKOA WA SINGIDA**

**HATI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA. 22/2023**

**OMBI LA STELLA JOHN KESSY**

**KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU PROSPER JASTIN SHIRIMA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote wa mirathi ya marehemu PROSPER JASTIN SHIRIMA wanaalikwa kuja Mahakamani kuhudhuria kesi wakiwa wanataka mnamo tarehe 4 Mwezi wa 9 Mwaka 2023 kabla mwombaji huyo hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Tarehe 16/8/2023

Hakimu Mkazi
Mahakama ya Wilaya Singida.

---

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA



Viongozi wa ngazi za juu kutoka mataifa mbalimbali duniani wakishiriki katika mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, jana. **PICHA MTANDAO.**

# Afrika yapaza sauti ukosefu usawa duniani

**NEW YORK, Marekani**

VIONGOZI kadhaa wa mataifa ya Afrika wamepaza sauti juu ya suala la ukosefu wa usawa duniani akiwemo Rais wa Rwanda, Paul Kagame ambaye amezungumzia mzozo wa madeni unavyoyatia kitanzi mataifa yanayoendelea na kuyapunguzia kasi ya kutimiza malengo ya maendeleo endelevu ikiwa ni pamoja na kutokomeza umasikini.

Viongozi hao walitoa hotuba jana katika siku ya pili ya mkutano wa kila mwaka wa hadhara kuu ya Umoja wa Mataifa (UN).

Alisema sababu ya hali hiyo ni kupandishwa viwango vya riba kwenye mataifa yaliyoendelea ambayo ndiyo wakopeshaji wakubwa wa nchi masikini.

Pia Rais Kagame alitumia hotuba yake kutoa rai ya mageuzi kwenye mifumo ya fedha ya kimataifa kuziwezesha nchi masikini kuifikia mitaji huku ikiwapa uhuru wa kupanga vipaumbele vyake vya maendeleo na matumizi ya rasilimali ilizonazo.

Wito wa aina hiyo ulitolewa pia na Rais wa visiwa vya Ushelisheli, Wavel Ramkalawan, ambaye alieleza kuwa ili mfumo wa ushirikiano na mshikamano ulimwenguni ufanye kazi kwa ufanisi, ni lazima kuwe na juhudi za pamoja na kubadilishana maarifa na uzoefu katika kuzishughulikia changamoto kubwa kama umasikini, ukosefu wa chakula na athari za uharibifu mazingira.

Aidha, alitoa wito kwa mataifa yanayoendelea chini ya mwamvuli unaofahamika kama muungano wa nchi za kusini mwa dunia, kushirikiana kwa kupeana ujuzi na kuwa mfano wa mabadiliko akisema Ushelisheli iko tayari kubadilishana uzoefu wake na nchi nyingine.

Rais wa Angola, Joao Lourenco, alikumbusha kuwa hata baada ya miaka 78 tangu kuundwa kwa Umoja wa Mataifa bado imesadifu kuwa vigumu kuzuia mifarakano duniani.

Kwa mujibu wa Lourenco, sababu za hayo yote ni kuendelea kukosekana usawa ulimwenguni baina ya nchi tajiri na zinazoendelea.

"Hali hiyo inayanyima fursa mataifa masikini kushiriki kwenye kutafuta ufumbuzi wa matatizo na mizozo inayotokea na kwa upande mwengine sauti ya nchi hizo hazisikilizwi," alisema.

Alibainisha kuwa mwenendo huo unazifanya nchi hizo kutotimiza matarajio ya umma ambapo baadaye inakuwa rahisi kushawishika kutumia njia zisizo za kiungwana kufanya mabadiliko kwa matumaini ya kutatua changamoto zilizomo kwenye mataifa yao.

Rais wa Ghana, Akufo-Addo, aligusia eneo hilo la ukosefu wa usawa kwenye jukwaa la kimataifa, akihoji juu ya sababu za Umoja wa Mataifa kutofanyiwa mageuzi hata baada ya karibu miongo minane tangu kuundwa kwake.

Eneo mojawapo ni muundo wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Rais Akufo-Addo, alisema muundo uliopo hauakisi ujumuishaji wa kila kanda ya dunia ikiwemo Afrika.

"Mfumo ulioko hauwezi kujenga imani ya chombo hicho kilicho na jukumu muhimu la kusimamia amani na utulivu duniani," alisema.

**FIDIA YA UTUMWA**

Rais Akufo-Addo, pia alitaka malipo ya fidia kwa mataifa ya Afrika kutokana na dhuluma za kihistoria za biashara ya utumwa iliyovuka Atlantiki.

Vile vile, alisisitiza kuwa huu ndio wakati wa kuweka mada ya ulipaji fidia mbele. Akisema dunia kwa karne nyingi haikuwa tayari na haiwezi kukabiliana na matokeo ya biashara ya utumwa.

Alisema "fidia lazima zilipwe" akiongeza kuwa ingawa hakuna fedha zinazoweza kufidia hali ya kutisha ya biashara ya utumwa, ingeleta hoja kwamba mamilioni ya Waafrika waliozalisha waliwekwa kazini bila kulipwa fidia.

Ilielezwa kuwa sio mara ya kwanza kwa rais wa Ghana kuzungumza kuhusu fidia, mwaka jana alisema muda ulikuwa umechelewa ili kuongeza mijadala kuhusu suala hilo.

Alitoa wito wa kuomba radhi rasmi kwa mataifa ya Ulaya ambayo yalihusika katika biashara hiyo, na kuutaka Umoja wa Afrika (AU) kuwashirikisha diaspora ili kuendeleza kazi ya fidia.

Kwa mujibu wa UN biashara ya watumwa iliyovuka Atlantiki, ambayo iliathiri mamilioni ya Waafrika, ilikuwa uhamiaji mkubwa zaidi wa kulazimishwa katika historia na moja ya unyanyasaji wa kibinadamu.

Kuhama kwa Waafrika kulienea katika maeneo mengi ya ulimwengu kwa kipindi cha miaka 400. Ghana ilikuwa mojawapo ya vituo vya kuondoka kwa wengi wa wale waliokuwa watumwa huko Afrika Magharibi.

**DW, BBC**

## Chanjo VVU kuanza majaribio Afrika Kusini

**JOHANNESBURG, Afrika Kusini**

AFRIKA Kusini na Marekani zinatarajia kuanza majaribio ya chanjo mpya ya kuzuia Virusi vya Ukimwi (VVU) na kwamba tayari zimeanza kuwaandikisha washiriki watakaoshiriki katika majaribio ya kimatibabu.

Kwa mujibu wa shirika la utafiti la serikali la Marekani la Taasisi za Kitaifa za Afya (NIH), chanjo hiyo, iitwayo VIR-1388, imeundwa kusaidia seli za T za mwili, zinazosaidia mfumo wa kinga kupambana na vijidudu na kukinga dhidi ya magonjwa.

Chanjo hiyo inakusudiwa kuelekeza mfumo wa kinga ya mwili kuzalisha T-seli zinazoweza kutambua VVU na kuashiria mwitikio wa kinga ili kuzuia virusi kuanzisha maambukizi ya muda mrefu.

Ilielezwa kuwa jaribio la chanjo hiyo linafadhiliwa na NIH, Wakfu wa Bill na Melinda Gates na kampuni ya Marekani ya Vir Biotechnology.

Pia ilibainishwa kuwa utafiti huo utaandikisha washiriki 95 wasio na VVU katika maeneo manne nchini Afrika Kusini na maeneo sita nchini Marekani.

Matokeo ya awali ya jaribio la chanjo yatatangazwa mwishoni mwa 2024, lakini baadhi ya washiriki wataendelea na majaribio kwa miaka mitatu.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa mwaka 2020, NIH ilisitisha majaribio ya chanjo nyingine ya VVU nchini Afrika Kusini baada ya ukaguzi kugundua kuwa chanjo hiyo haikuwa na ufanisi katika kuzuia maambukizi ya VVU.

**BBC**

**Chanjo hiyo inakusudiwa kuelekeza mfumo wa kinga ya mwili kuzalisha T-seli zinazoweza kutambua VVU na kuashiria mwitikio wa kinga ili kuzuia virusi kuanzisha maambukizi ya muda mrefu...**

# Dola Bil 11.6 kujenga upya makazi Morocco

**RABAT, Morocco**

MFALME wa Morocco Mohammed VI, amesema nchi yake itatumia Dola Bilioni 11.6 kwa ajili ya kujenga upya maeneo yaliyoharibiwa baada ya tetemeko la ardhi la tarehe nane ya mwezi huu.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, pesa hizo pia zitatumika kuwasaidia zaidi ya watu milioni 4.2 katika majimbo yaliyoathirika pakubwa na tetemeko hilo la ardhi.

Watu waliopoteza makazi yao wanatarajiwa kujengewa makao mapya, miundombinu iliyoharibika katika mkasa huo pia ikitarajiwa kufanyiwa marekebisho katika kipindi cha zaidi ya miaka mitano.

Alibainishwa kuwa zaidi ya watu 2,900 waliuawa katika tetemeko la ardhi lenye uzito wa 6.8 wakati wengine zaidi ya 5,000 wakiripotiwa kujeruhiwa.

Aidha, ilielezwa kuwa hilo ndilo limekuwa tetemeko kubwa zaidi la ardhi kuwahi kutokea nchini Morocco katika kipindi cha zaidi ya miaka 60.

**RFI**

HABARI KITAIFA

# MUDATHIR AFUNGUKA SIRI YA KUIFUNGIA YANGA BAO

Na Saada Akida

KIUNGO wa Yanga, Mudathir Yahya amesema baada ya kuona wanapoteza nafasi nyingi za kufunga katika mchezo wa juzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamond, alimuinua benchi na kumpa maelekezo 'maalum' ya kusaka ushindi ambayo yalizaa matunda.

Mudathir aliingia uwanjani dakika ya 67 pamoja na Jesus Moloko wakichukua nafasi za Clement Mzize na Pacome Zouzoua.

Kiungo huyo aliifungia Yanga bao pekee zikiwa zimebaki dakika mbili kabla ya filimbi ya mwisho katika mechi hiyo ya raundi ya tatu iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex.

"Kocha aliniambia nihakikishe tukiwa tunashambulia muda wote nakaa kwenye boksi la wapinzani wetu, nilifanya hivyo na mpira ulipokuja nilitumia ujanja kuugusa na kutinga nyavuni, nashukuru timu imepata ushindi muhimu," alisema Mudathir.

Aliongeza anafurahi kuona ametekeleza majukumu aliyopewa na kocha wake baada ya kuona wachezaji wenzake wamepoteza nafasi nyingi za kufunga na dakika zikiwa zimeyoyoma.

Nyota huyo amewaita mashabiki wa Yanga kujitokeza kwa wingi katika mchezo wa marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Merrikh kutoka Sudan utakaochezwa Septemba 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex.

"Tunawahakikishia siku ya Septemba 30 watafurahi, waje kwa wingi katika mchezo wetu wa marudiano dhidi ya Al Merrikh, tutapambana kuhakikisha tunafuzu kucheza hatua ya makundi, tena kwa kishindo," alisema Mudathir.

Yanga itarudiana na Al Merrikh huku ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-0 walioupata katika mechi ya kwanza iliyochezwa Kigali, Rwanda wiki iliyopita.

Nyota huyo alifunga bao kufuatia pasi ya Moloko kwa kupenyeza mguu katikati ya mlinzi wa Namungo, Derrick Mukombozi na kuugusa mpira uliomshinda golikipa, Deogratius Munishi 'Dida' na kuibua shangwe kwa mashabiki wa timu hiyo.



Wasichana wanaolelewa katika kituo cha michezo cha JKM Park kilichoko Dar es Salaam wakifanya mazoezi ili kujiimarisha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Twiga Stars kibaruani leo

Na Saada Akida

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake 'Twiga Stars' inatarajia kucheza dhidi ya wenyeji Ivory Coast katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON 2024) itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Yamoussokro nchini humo.

Nyota wote wa Twiga Stars wanaocheza soka la kulipwa wameshaungana na wenzao tayari kwa ajili ya mchezo huo na ule wa marudiano utakaofanyika Septemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kuelekea mchezo huo wa leo Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo na malengo yake ni kupata ushindi ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele.

Shime alisema hawafahamu vizuri wapinzani wao lakini amekiandaa vyema kikosi kucheza soka la ushindani na anaamini watafanikiwa.

"Tuna mipango mitatu ambayo tutaingia nayo katika mchezo wa kesho (leo), kwa sababu hatuwafahamu vizuri Ivory Coast, kwa mikakati tutakayoingia nayo nina matumaini ya kufanya vizuri," alisema Shime.

Aliongeza wachezaji wake wameahidi wataipeperusha vyema bendera ya Tanzania baada ya kufanyia kazi makosa ya mwaka jana wakati walipocheza dhidi ya Namibia.

## JKT, Kagera Sugar kuvaana Shinyanga

Na Adam Fungamwango

TIMU ya JKT Tanzania itaanza rasmi kuutumia Uwanja wa CCM Kambarage ulioko Shinyanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Kagera Sugar itakayochezwa Septemba 29, mwaka huu, imefahamika.

Mechi hiyo itakuwa ni ya kwanza ya nyumbani kwa JKT Tanzania na inatokana na kukamilika kwa maboresho kama walivyoshauriwa na Bodi ya Ligi.

Mwenyekiti wa timu hiyo, Kapteni Godwin Ekingo, amesema kikosi chao kilitarajiwa kufika Shinyanga jana usiku kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya mechi hiyo ya raundi ya tatu.

"Timu imeshatoka Dar itawasili Shinyanga muda wowote, tuliomba hapa kuwa ndiyo uwanja wetu wa nyumbani," alisema Ekingo ambaye timu yake ina pointi tatu ilizopata ugenini katika mechi ya kwanza dhidi ya Namungo.

Naye Meneja wa Uwanja wa CCM Kambarage, Lawrence Manotta, alisema uwanja huo kwa sasa upo tayari kutumika baada ya kukamilisha maboresho ambayo walitakiwa kuyafanya.

## Serengeti Girls kuivaa Morocco

Na Saada Akida

KOCHA Msaidizi wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), Esther Chabruma amesema kikosi chake kiko tayari kwa ajili ya mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Morocco itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Chabruma aliliambia gazeti hili wanaamini mechi hiyo itawasaidia kuwajenga na kuwaweka tayari na michezo ya kuwania nafasi ya kushiriki fainali zijazo za U-17 za Afrika na Kombe la Dunia.

"Timu yangu ni changa, ni wachezaji tumewachukua kutoka katika ligi ndogo, bado ni wachanga, tunaendelea kuwaandaa ili kuelekea mechi dhidi ya Morocco," alisema Chabruma.

Naye Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, amesema wanashukuru kupata mechi mbili za kirafiki dhidi ya Morocco na anaamini zitawaimarisha nyota wake kuelekea michuano ijayo.

Kidao alisema huu ni mwanzo wa kuijenga timu hiyo na watatafuta michezo mingine ya kirafiki kwa ajili ya kufikia malengo ya kuiandaa vyema Serengeti Girls.

## ZISIKUPITE

### SANCHO BASI TENA
KLABU ya Borussia Dortmund haina nia ya kumnunua tena winga wa Manchester United na England Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23. **(Bild)**

### RODRYGO AWANIWA L'POOL
LIVERPOOL ina nia ya kumsajili winga wa Real Madrid na Brazil, Rodrygo mwenye umri wa miaka 22 ikiwa mshambiliaji wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31 ataamua kuhama katika klabu hiyo Januari. **(Fichajes)**

### PALHINHA HANA KIPENGELE
KIUNGO wa Fulham na Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 28 hana kipengele cha kuachiliwa katika mkataba wake mpya.**(Football Insider)**

### BARCO NA MAN CITY
KLABU ya Manchester City inaweza kumpata beki wa Boca Juniors na Argentina, Valentin Barco mwenye umri wa miaka 19 kwa ada ya takriban pauni milioni 15 Januari. **(Football Insider)**

### CHELSEA DILI KUBWA
CHELSEA inatazamiwa kupokea dau la pauni milioni 400 kutoka kwa kampuni ya uwekezaji ya Ares Management yenye makao yake makuu nchini Marekani kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wao mpya na miradi mingine. **(Telegraph)**

### SON MKATABA MPYA
KLABU ya Tottenham Hotspur Spurs iko tayari kumpa mshambuliaji wa Korea Kusini, Son Heungmin mwenye umri wa miaka 31 mkataba mpya na kuongeza muda wake wa kusalia London kaskazini hadi mwaka 2025. **(90min)**

### MUKASA AWANIWA CITY
MANCHESTER City inatazamiwa kumsajili kiungo wa kati wa England chini ya umri wa miaka 17, Divine Mukasa mwenye miaka 16, kutoka West Ham. **(Fabrizio Romano)**

### CITY ILIKATAA OFA
KLABU ya Manchester City ilikataa ofa ya mkopo kwa mshambuliaji wa Norway, Oscar Bobb mwenye umri wa miaka 20 kutoka Ajax na Porto. **(Telegraph)**

### EKITIKE ATAKA KUBAKI
MCHEZAJI wa Paris St-Germain, Hugo Ekitike mwenye umri wa miaka 21 yuko tayari kupigania mustakabali wake katika klabu ya mabingwa hao wa Ufaransa, lakini mshambuliaji huyo wa Ufaransa anafahamu klabu za Ligi Kuu ya England, Crystal Palace, Brentford, Everton, West Ham United na Wolves vina nia ya kumsajili. **(90 Min)**

### MOORE AWINDWA
KLABU ya Huddersfield Town inatazamiwa kumteua kocha wa zamani wa Sheffield Wednesday, Darren Moore mweye umri wa miaka 49, kama kocha wao mpya baada ya kuachana na Neil Warnock. **(Sun)**

### MONTELLA KOCHA UTURUKI
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Italia, Vincenzo Montella mwenye umri wa miaka 49 anatazamiwa kuteuliwa kuwa kocha mkuu wa Uturuki. **(Fabrizio Romano)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ONANA: NILAUMIWE MIMI KUFUNGWA MAN UNITED

●●●Ni kufuatia kipigo walichokipata mbele ya Bayern Munich, amekiri kuwa...

**MUNICH, Ujerumani**

GOLIKIPA Andre Onana amesema anapaswa kulaumiwa yeye baada ya Manchester United kufungwa na Bayern Munich kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, huku akikiri kwamba mwanzo wa maisha yake ya soka Old Trafford umekuwa "si mzuri sana."

Onana alifanya makosa kuipa Bayern bao la kuongoza katika Uwanja wa Allianz Arena na kumfanya Leroy Sane kufunga kwenye mchezo huo.

United hatimaye walipoteza 4-3 na kufanya kuwa vipigo vitatu mfululizo kwa vijana wa Erik ten Hag.

"Tulianza vizuri sana na baada ya kosa langu tulipoteza udhibiti wa mchezo," alisema Onana.

"Ni hali ngumu kwangu, niliishusha timu. Ni kwa sababu yangu hatukushinda mchezo huu. Tunapaswa kusonga mbele, ni maisha ya golikipa."

Onana amekuwa na mwanzo mgumu wa maisha ndani ya United kufuatia uhamisho wake wa pauni milioni 47 kutoka Inter Milan majira ya joto.

Kipa huyo wa Cameroon tayari amelaumiwa kwa mabao dhidi ya Nottingham Forest, Arsenal na Brighton na usiku wa kuamkia jana dhidi ya Bayern alikiri kwamba kuchukua nafasi ya David de Gea "si kitu rahisi."

Baada ya makosa yake dhidi ya Bayern, Onana aliomba kutimiza ahadi za vyombo vya habari vya United baada ya mechi ili kuomba msamaha kwa kosa lake.

"Hawakuwa wametengeneza nafasi yoyote, shuti lao la kwanza lililolenga goli nilifanya makosa na timu ikashuka," alisema.

"Tulipambana hadi mwisho lakini lazima nitambue kuwa hatukushinda kwa sababu yangu. Bado nina mengi ya kuthibitisha kwa mashabiki. Mwanzo wangu haukuwa mzuri sana, sio jinsi nilivyotaka. Ni ngumu. Ilikuwa ni fursa ya kurudi nyuma na ndio, ni wakati mgumu, wakati mgumu na inabidi tuwe pamoja na kujifunza kutokana na makosa yetu.

"Ni jukumu langu, kwa sababu yangu hatukushinda na lazima nijifunze kutoka kwake.

"Nina mengi ya kuthibitisha, kwa sababu kusema ukweli mwanzo wangu Man United sio mzuri sana. Ni mimi niliyeiangusha timu."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,154,8
MECHI KALI
MONACO
VERSUS
NICE
1 | 2.09
X | 3.81
2 | 3.24
tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Shabani Mbegu - 0652 322 XXX
2. Mpenja Mwahalende - 0652 555 XXX
3. Hadinani Ungite - 0655 714 XXX
4. Abdallah Juma - 0677 452 XXX
5. Deogratius Kessy - 0713 325 XXX
6. Aweso Jaribuaweso - 0715 458 XXX
7. Florence Florence - 0715 792 XXX
8. Brighton Gerald - 0715 906 XXX
9. Hamisi Saidi - 0719 775 XXX
10. Faki Hamisi - 0779 457 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NACHO- BELLINGHAM ALIZALIWA KUCHEZA REAL MADRID



**MADRID, Hispania**

NAHODHA wa Real Madrid, Nacho amesema Jude Bellingham "alizaliwa kuichezea Real Madrid" baada ya bao la sita la kiungo huyo katika mechi sita kuwapa wababe hao wa LaLiga ushindi wa 1-0 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Union Berlin katika mchezo wao wa ufunguzi wa Kundi C.

Bellingham aliuwahi mpira uliozagaa ndani ya eneo la yadi sita katika dakika ya 94 Jumatano usiku huko Santiago Bernabeu baada ya shuti la Federico Valverde kupanguliwa na kufunga bao hilo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England amefunga katika mechi tano kati ya sita alizoicheza Real Madrid hadi sasa.

"Nadhani Jude alizaliwa kuichezea Real Madrid," nahodha wa klabu hiyo Nacho aliiambia Movistar.

"Tuna bahati kuwa naye hapa pamoja nasi. Tutegemee ataendelea kufunga mabao."

Goli la Bellingham dhidi ya Union Berlin lilikuwa ni mara yake ya pili kushinda mchezo kwa Madrid katika muda wa nyongeza katika Uwanja wa Bernabeu, baada ya bao lake la ushindi dakika ya 95 dhidi ya Getafe mnamo Septemba 2.

"Tulikuwa na subira," alisema Bellingham akiiambia Movistar.

"Tulijua tungepata nafasi mwishoni mwa mchezo. Tulilazimika kusonga na mpira, kutafuta nafasi. Tuliendelea, tulionyesha mawazo mazuri na umoja mkubwa."

Bellingham alifunga mabao 14 kwa Borussia Dortmund katika msimu uliopita, na tayari sasa hivi ameshafunga mabao sita katika msimu wake wa kwanza Bernabeu.

"Ndani ya uwanja nataka kuwa mchezaji, nataka kujaribu kutengeneza vitu kwa wachezaji wenzangu, lakini mpira unapoingia kwenye boksi nataka kuwa muuaji," alisema.

"Hilo ndilo litakalotushindia michezo. Tunatumahi tutaendelea hivi.

# Solskjaer akiri ilikuwa kosa kumsajili Ronaldo

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amekiri kwamba uamuzi wa kumrejesha Cristiano Ronaldo katika klabu ya Manchester United wakati alipokuwa kocha "uligeuka kuwa mbaya."

Kurejea kwa Ronaldo kwa United Agosti 2021 hakufanikiwa kufikia matarajio huku Mreno huyo akiondoka katika mazingira magumu na kujiunga na Al Nassri ya Saudi Arabia.

"Ulikuwa uamuzi ambao ulikuwa mgumu sana kuukataa na nilihisi kwamba tulipaswa kuuchukua, lakini ikawa si sawa," alisema Solskjaer katika mahojiano na The Athletic.

"Nilijisikia vizuri sana aliposaini na mashabiki walihisi hivyo kwenye mchezo na Newcastle, wakati Old Trafford ilipotikisa kwa Ronaldo kufunga mara mbili katika ushindi wa 4-1.

"Bado alikuwa mmoja wa wafungaji bora zaidi duniani, alikuwa akionekana kuwa na nguvu."

Raia huyo wa Norway alisema anamuonea huruma kocha wa sasa Erik ten Hag ambaye anakabiliwa na shinikizo baada ya kuanza vibaya msimu huu.

United wamepoteza mechi tatu kati ya tano za mwanzo za Ligi Kuu ya England.

Solskjaer, ambaye alifutwa kazi Novemba 2021 baada ya kuiongoza kwa chini ya miaka mitatu tu huku kukiwa na matokeo mabaya, alisema kusimamia klabu hiyo ya Old Trafford ni changamoto hasa ikizingatiwa kwamba ulinganisho hufanywa moja kwa moja na utawala wa Alex Ferguson uliobeba mataji.

"Ninajua anachopitia. Ni kazi ya ndoto, lakini ni ngumu," alisema Solskjaer.

"Unashughulika na wanadamu wenye matatizo na asili zao zote, huu si uigaji wa kompyuta. Lakini wachezaji wengi ni wataalamu wazuri ambao wanataka kufanya vyema. Wengine hufikiria kuhusu namba moja kwanza, wengi hufikiria klabu. "

Solskjaer alisema United sasa inatatizika kusajili aina ya wachezaji ambao hapo awali wangehitaji ushawishi mdogo wa kujiunga, akisema klabu hiyo imekosa malengo muhimu kama kushindwa kuwatwaa Jude Bellingham, Harry Kane na Declan Rice.

"Matarajio ni makubwa sana lakini hatuwezi kuishi enzi sawa na nilipocheza," alisema.

"Tulikuwa na Arsenal na Chelsea kama wapinzani kuelekea mwisho. Sasa, timu nyingi zina fedha au hata kama hazina, hazihitaji kuuza.

"Hapo zamani, Wayne Rooney na Cristiano walikuwa wachezaji bora chipukizi na tuliwasajili. Sasa, United haiwezi tu kwenda kumnunua mshambulizi wa Brighton, Evan Ferguson.

"Hatukuweza kununua wachezaji niliowataja kwa klabu. Tulimtaka Jude Bellingham, lakini naheshimu alichagua Dortmund. Labda hiyo ilikuwa busara."

## HABARI MICHEZO


361,566/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/09/23 | 17:00 | Middlesbrough FC vs Southampton FC | 2.65 | 3.35 | 2.47 |
| 02. 23/09/23 | 17:00 | Dundee FC vs Kilmarnock FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 03. 23/09/23 | 17:00 | Airdrieonians FC vs Raith Rovers FC | 2.43 | 3.20 | 2.55 |
| 04. 23/09/23 | 17:15 | CA Osasuna vs Sevilla FC | 2.50 | 3.20 | 2.70 |
| 05. 23/09/23 | 19:30 | Burgos CF vs Elche CF | 2.80 | 3.00 | 2.60 |
| 06. 23/09/23 | 19:30 | Werder Bremen vs FC Cologne | 2.55 | 3.50 | 2.50 |
| 07. 23/09/23 | 19:45 | NEC Nijmegen vs FC Utrecht | 2.55 | 3.55 | 2.47 |
| 08. 23/09/23 | 20:00 | Casa Pia Lisbon vs Vitoria SC Guimaraes | 2.55 | 3.05 | 2.80 |
| 09. 23/09/23 | 22:00 | Stade Brest 29 vs Olympique Lyon | 2.55 | 3.50 | 2.50 |
| 10. 24/09/23 | 14:00 | FC Metz vs Strasbourg Alsace | 2.85 | 3.20 | 2.42 |
| 11. 24/09/23 | 15:30 | Ajax Amsterdam vs Feyenoord Rotterdam | 2.48 | 3.60 | 2.50 |
| 12. 24/09/23 | 17:00 | Cercle Brugge vs Union Saint-Gilloise | 2.65 | 3.40 | 2.45 |
| 13. 24/09/23 | 17:15 | Real Oviedo vs Real Valladolid | 2.75 | 2.85 | 2.70 |
| 14. 24/09/23 | 17:15 | Rayo Vallecano vs Villarreal CF | 2.55 | 3.40 | 2.55 |
| 15. 24/09/23 | 18:05 | Montpellier HSC vs Stade Rennes | 2.65 | 3.45 | 2.43 |
| 16. 24/09/23 | 21:45 | Torino FC vs AS Roma | 2.85 | 2.95 | 2.55 |
| 17. 24/09/23 | 22:00 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.65 | 3.35 | 2.47 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 22/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4332 | Qatar U23 vs Palestine U23 | 1.43 | 3.92 | 6.93 |
| 18:00 | 1532 | AL Akhdood vs Al Khaleej Club | 2.59 | 3.35 | 2.59 |
| 18:00 | 1856 | Ben Aknoun vs ASO Chlef | 3.00 | 3.05 | 2.28 |
| 18:00 | 1922 | AL Riyadh vs AL Faiha | 2.63 | 3.36 | 2.55 |
| 18:00 | 2796 | CS Constantine vs MC Alger | 2.00 | 3.00 | 3.76 |
| 18:30 | 1689 | Domzale vs NK Aluminij | 1.74 | 3.69 | 3.79 |
| 19:00 | 2666 | Spartak Subotica vs FK Vozdovac | 2.19 | 3.03 | 3.08 |
| 19:30 | 1034 | BATE Borisov vs Belshina | 1.14 | 7.17 | 12.30 |
| 19:30 | 1963 | Salernitana vs Frosinone | 2.45 | 3.25 | 2.99 |
| 19:45 | 4032 | Flora Tallinn vs Tallinna Kalev | 1.20 | 5.31 | 12.25 |
| 20:00 | 3850 | Lyngby vs Vejle BK | 1.88 | 3.51 | 3.86 |
| 20:00 | 4047 | Gaziantep BB vs Istanbulspor | 2.05 | 3.46 | 3.25 |
| 20:30 | 3580 | Red Star vs Avranches | 1.61 | 3.87 | 4.85 |
| 21:00 | 1114 | Al Nasr Riyadh vs Al Ahli Jeddah | 1.77 | 3.82 | 4.13 |
| 21:00 | 1503 | Roda Kerkrade vs Den Bosch | 1.43 | 4.40 | 5.93 |
| 21:00 | 1865 | NAC Breda vs Emmen | 2.17 | 3.52 | 2.86 |
| 21:00 | 2572 | JS Kabylie vs Paradou AC | 1.86 | 3.21 | 3.97 |
| 21:00 | 3245 | Jong PSV vs VVV Venlo | 2.87 | 3.64 | 2.12 |
| 21:00 | 3305 | Jong Utrecht vs Cambuur | 4.39 | 3.93 | 1.63 |
| 21:00 | 4243 | Al Wehda vs Abha | 1.78 | 3.77 | 4.13 |
| 21:00 | 4817 | Dordrecht vs Jong AZ Alkmaar | 2.24 | 3.49 | 2.77 |
| 21:00 | 4937 | FK Zeleznicar Pancevo vs Partizan | 6.83 | 4.12 | 1.39 |
| 21:00 | 5561 | GO Ahead Eagles vs Fortuna Sittard | 2.02 | 3.57 | 3.17 |
| 21:00 | 5783 | ADO Den Haag vs Telstar | 1.64 | 3.95 | 4.31 |
| 21:00 | 5882 | Helmond Sport vs Groningen | 3.94 | 3.63 | 1.77 |
| 21:15 | 2078 | FC Thun vs FC Aarau | 1.89 | 3.69 | 3.23 |
| 21:30 | 3893 | Palermo vs Cosenza | 1.63 | 3.64 | 4.93 |
| 21:30 | 3969 | LKS Lodz Pss vs Jagiellonia | 2.52 | 3.08 | 2.57 |
| 21:30 | 4109 | Lechia Gdansk vs GKS Katowice | 2.20 | 3.33 | 2.82 |
| 21:30 | 5648 | Rangers vs Santiago Morning | 2.07 | 3.16 | 3.32 |
| 21:30 | 5752 | Stuttgart vs SV Darmstadt | 1.47 | 4.61 | 6.52 |
| 21:45 | 1429 | Newry City AFC vs Dungannon Swifts | 2.72 | 3.33 | 2.26 |
| 21:45 | 1697 | Shelbourne vs Cork City | 1.58 | 3.48 | 5.24 |
| 21:45 | 2217 | Larne vs Carrick Rangers | 1.22 | 5.45 | 9.29 |
| 21:45 | 2344 | Lecce vs Genoa | 2.34 | 3.18 | 3.24 |
| 21:45 | 3112 | St Patricks vs Dundalk FC | 2.00 | 3.28 | 3.28 |
| 21:45 | 3243 | UCD Dublin vs Shamrock Rovers | 18.17 | 7.27 | 1.09 |
| 21:45 | 3442 | Standard Liege vs KVC Westerlo | 1.86 | 3.74 | 3.59 |
| 21:45 | 3559 | Glentoran Belfast vs Coleraine FC | 1.59 | 3.63 | 4.84 |
| 21:45 | 4450 | Sligo Rovers vs Derry City | 3.78 | 3.27 | 1.85 |
| 21:45 | 4615 | Drogheda Utd vs Bohemians FC | 3.67 | 3.42 | 1.83 |
| 21:45 | 4930 | Cardiff Met Uni. vs The New Saints | 7.47 | 4.95 | 1.29 |
| 21:45 | 5161 | Queens Park vs Ayr United | 1.94 | 3.47 | 3.42 |
| 22:00 | 1121 | Admira Wacker vs SKN St Polten | 2.90 | 3.41 | 2.17 |
| 22:00 | 2303 | Alaves vs Athletic Bilbao | 3.56 | 3.10 | 2.24 |
| 22:00 | 3158 | Monaco vs Nice | 2.09 | 3.81 | 3.24 |
| 22:00 | 3910 | Aberystwyth Town vs Penybont | 4.44 | 4.23 | 1.54 |
| 22:00 | 5017 | FC Cartagena vs Eibar | 3.07 | 3.02 | 2.31 |
| 22:00 | 5337 | Birmingham vs QPR | 1.88 | 3.37 | 3.82 |
| 22:15 | 5096 | Famalicao vs FC Arouca | 2.02 | 3.24 | 3.54 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# SIMBA : KAPOMBE, ZIMBWE JR BADO WAKO KATIKA UBORA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema wachezaji wake, Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' bado wako katika ubora wao na hawajachoka kama baadhi ya wadau soka nchini wanavyoeleza, imefahamika.

Simba imelazimika kutoa ufafanuzi huo kufuatia hoja iliyochangiwa na kocha na mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Jamhuri Kihwelo 'Julio' ambaye alisema mabeki hao wamechoka na ni muda sahihi kwa David Kameta 'Duchu' na Israel Mwenda kupewa nafasi.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wachezaji hao wamecheza kwa muda mrefu hivyo inaonekana mashabiki wamewachoka na si kweli wameshuka viwango.

"Watu wamewachoka Kapombe na Tshabalala (Zimbwe Jr), sasa wanawasingizia wamechoka, hoja hii imeshamiri baada ya mechi ya Power Dynamos.

"Kuna wakati watu walimchoka, Juma Kaseja na kila siku akawa anaulizwa unastaafu lini, sio kwa sababu alishuka kiwango lakini walichoka kumwona, nchi hii Kapombe na Tshaba bado wana muda zaidi wa kucheza kulingana na ubora wao, hivyo ni jukumu letu Wana-Simba kuwalinda vijana hawa ambao ni tunu ya taifa," alisema Ahmed.

Aliongeza timu nyingine hapa nchini zimehangaika kupata mabeki wa kulia na kushoto, lakini kwa muda mrefu klabu yao imekaa salama kwenye maeneo hayo.

"Tunao vijana wengine katika maeneo hayo (Duchu na Mwenda), ambao taratibu watarithi mikoba hiyo kwa wakati husika, lakini tukitaka kuwarithisha kwa presha tutaambulia presha," aliongeza.




Mshindi wa Jackpot bonus kutoka SportPesa, Pendo Mwakyangula akishikilia hundi ya mfano baada ya kubashiri kwa usahihi baadhi ya mechi za Jackpot. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Gamondi: Muhimu kupata pointi tatu

INATOKA UK. 24

mechi hiyo kwa sababu alipoteza pointi lakini hakuna anachowadai wachezaji wake kutokana na walivyopambana na kutoruhusu kufungwa idadi kubwa ya mabao.

"Siwadai wachezaji wangu, wamejitahidi tumefanya makosa dakika 20 za mwisho na kutuadhibu kwa kuruhusu bao, tulitengeneza nafasi nyingi za wazi, hii inatokana na kukos ubunifu na pasi za mwisho na kushindwa kufanyia kazi kupata bao.

Hii inachangia kukosa wachezaji wenye ubora wa kutosha katika eneo la ushambuliaji, na kwa kiwango wachezaji walichoonyesha katika mechi hii imenipa mwanga mzuri wa ubora wa kikosi changu tunapoelekea kwenye mechi zijazo," alisema Kaze.

Mrundi huyo aliongeza hakuna sehemu yoyote iliyoandikwa kwenye kitabu cha dini Yanga lazima atashinda bao tano au atafunga idadi hiyo ya mabao.

# SIMBA SC YAIRARUA COASTAL

INATOKA UK. 24

Coastal Union kuwabana Simba ambao licha ya kumiliki mpira na kutengeneza nafasi walishindwa kuongeza bao lingine katika kipindi cha pili.

Simba pia ilifanya mabadiliko manne kwa mkupuo dakika ya 72 ya mchezo kwa kuwatoa Shomari Kapombe, Baleke, Mzamiru Yassin na Ntibazokinza na nafasi zao kuchukuliwa na Israel Mwenda, Kibu Denis, Sadio Kanoute na Willy Onana.

Hata hivyo mabadiliko hayo hayakubadili matokeo ya mchezo huo huku Coasta Union nao licha ya kuwa pungufu walikuwa wakijaribu kufanya mashambulizi lakini yalishia kwenye idara ya ulinzi ya Simba na kufanya kipa, Ayoub Lakred kuwa mapumziko kwa muda mrefu.

Michezo

Ijumaa Septemba 22, 2023

Nipashe



Onana: Nilaumiwe mimi kufungwa Man United UKURASA 21

# SIMBA SC YAIRARUA COASTAL

## ●●●Baleke akipiga 'hat trick' ya pili msimu huu, hali ya Inonga...

**Na Faustine Feliciane**

MSHAMBULIAJI Jean Baleke aliweka mambo sawa kati yake na mashabiki wa Simba baada ya kufunga hat katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania dhidi ya Coastal Union ambapo yake ilipata ushindi wa mabao yote yakifungwa kipindi cha kwanza.

Hata hivyo katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Simba ilipata pigo dakika ya 19 kufuatia beki wake, Henock Inonga kuchezewa rafu mbaya na Haji Ugando aliyelimwa kadi nyekundu ya moja kwa moja na mwamuzi, Ahmed Arajiga kutoka Manyara.

Rafu hiyo ilimfanya Inonga kukimbizwa katika hospitali ya Temeke na gari maalumu la kubebea wagonjwa lililokuwa uwanjani hapo na nafasi yake kuchukuliwa na Kenedy Juma.

Taarifa zilizopatikana baada ya kumalizika kwa mechi hiyo zilisema Inonga anaendelea vizuri na hajavunjika mguu kama hofu kubwa ya mashabiki ilivyotanda.

Baleke ambaye katika mchezo uliopita wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos alilaumiwa na baadhi ya mashabiki kwa kupoteza nafasi nyingi za kufunga, jana alianza kuwajibu mashabiki hao katika dakika ya sita tu kwa kufunga bao la kwanza akiunganisha pasi ya Clatous Chama.

Baada ya bao hilo Simba iliendelea kuishambulia Coastal Union na iliwachukua dakika tano kuandika bao la pili baada ya Baleke kuunganisha pasi ya pembeni kutoka kwa nahodha wa mchezo huo, Mohamed Hussein 'Zimbwe JR' aliyeuwahi mpira uliotemwa na golikipa, Chuma Hussein kufuatia shuti kali la Saido Ntibazokinza.

Simba iliendelea kulisakama lango la Coastal Union na dakika ya 38 Baleke alihitimisha karamu ya magoli kwa kufunga bao la tatu kwa penalti iliyotokana na Luis Miquissone kuangushwa ndani ya eneo la hatari akiwa anajiandaa kupiga shuti kuelekea langoni mwa Wagosi Wakaya.

Mpaka kipindi cha kwanza kinamalizika Simba walitoka uwanjani na idadi hiyo ya mabao ambapo yaliwapa ushindi na kufikisha pointi tisa sawa na vinara, Yanga wenye idadi nzuri ya mabao ya kufunga.

Kipindi cha pili kocha wa Coastal Union, Mwinyi Zahera alifanya mabadiliko na kubadli mfumo wa uchezaji huku wachezaji wake wakitumia muda mwingi kujihami na kushambulia kwa kushtukiza.

Nidhamu ya kujilinda iliwasaidia

UKURASA. 23



Kiungo wa Simba, Saido Ntibazonkiza (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Coastal Union katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Gamondi: Muhimu kupata pointi tatu

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kupata ushindi finyu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC iliyochezwa juzi, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema hana presha yoyote na jambo muhimu kwake lilikuwa ni kuondoka na pointi tatu muhimu.

Yanga ilipata ushindi wa bao 1-0, goli likifungwa dakika ya 87 na kuonekana mabingwa hao watetezi walibanwa baada ya kuvuna idadi kubwa ya magoli katika mechi zake mbili zilizopita.

Gamondi alisema hayo kwa upande wake hakuwa presha kwa sababu anatambua haitawezekana kila timu wanayokutana nayo kufunga mabao mengi.

Alisema ushindi huo pia hautawapa presha yoyote kuelekea mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Merrikh ambayo itachezwa wiki ijayo zaidi ya kuendelea kupata mwanga na kujipanga upya.

"Kikubwa tumepata pointi tatu katika mechi yetu ya leo (juzi), ilikuwa ngumu, Namungo FC wamecheza vizuri na ukizingatia wachezaji wangu wamepambana na kuondoka na ushindi wa bao 1-0. Ni kweli timu yangu imecheza taratibu, inawezakana ni uchovu lakini tulitengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia kwa wakati," alisema Gamondi.

Aliongeza kila timu wanayokutana nayo huja na mipango yake na Namungo walifanikiwa katika malengo yao hasa dakika 45 za kwanza.

Kocha huyo aliongeza alimpa jukumu kiungo wake, Mudathir Yahya la kufanyia kazi makosa ambayo yalifanywa na kiungo aliyetangulia ikiwamo kutumia nafasi aliyopata na kufunga goli na ushindi.

Naye Kocha Mkuu wa Namungo, Cedric Kaze alisema hakufurahia matokeo ya

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >